# MADA

## UHAKIKI WA MAUDHUI TEULE KATIKA *UTENZI WA NABII ISA*

**NA**

**OWALLAH KENNEDY OUMA.**
**C50/71961/2011.**

**TASNIFU HII IMETOLEWA ILI KUTOSHELEZA BAADHI YA MAHITAJI YA SHAHADA YA UZAMILI (M.A) KATIKA CHUO KIKUU CHA NAIROBI.**

**IDARA YA ISIMU NA LUGHA.**

**2013**

# UNGAMO.

Tasnifu hii ni kazi yangu mwenyewe na imetolewa kwa mahitaji ya shahada ya Uzamili (MA) katika Chuo Kikuu cha Nairobi na haijawahi kutolewa kwa mahitaji ya shahada katika chuo kikuu chochote.

------------------------------------------ Tarehe----------------------

Owallah Kennedy Ouma.

Tasnifu hii imetolewa kutahiniwa kwa idhini yetu tukiwa wasimamizi wa kazi hii wa Chuo kikuu Cha Nairobi.

Prof. Kineene wa Mutiso.

Sahihi ------------------------. Tarehe ---------------------.

Dkt. Tom Olali.

Sahihi --------------------------. Tarehe----------------------.

# TABARUKU

Kazi hii ninaitabarukia mke wangu Bi. Everlyne Awuor Ouma, ambaye aliweza kutambua umuhimu wa masomo katika jamii ya kisasa. Alijitolea mhanga kwa moyo wake mkunjufu na kuhakikisha kuwa nimeendeleza na kukamilisha masomo yangu.

Pia ninatabarukia baba yangu mpendwa Richard Owallah Anyango, mama yangu Joyce Achieng Owallah, marehemu babu yangu aliyenionyesha mwangaza katika masomo, binamu yangu Kenneth Magawi na ndugu zangu wote kwa kunipa msingi bora wa elimu na motisha katika masomo yangu bila kuchelea.

Aidha, sitasahau watoto wangu Dellice, Tatiana na Heyden ambao, walivumilia kwa muda mrefu ambao sikushikirikiana nao kwa mambo mengi kila mara waliponihitaji. Wote ninawaombea waweze kutambua dhima ya masomo katika maisha ya binadamu siku za leo na hata baadaye.

# SHUKRANI

Ningependa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa siha njema na fursa nzuri ya kuendeleza masomo yangu vilivyo, kwani bila yeye singefika nilipo sasa. Neema zake zilinifaa zaidi.

Nimeweza kutimiza kazi hii kwa ukarimu, juhudi na hisani za watu wengi ambao ningependa kuwataja baadhi yao kwa msaada, wema na uadilifu wao. Ushauri wao uliwezesha kazi hii kufikia kiwango hiki.

Ningependa zaidi kuwatolea wasimamizi wangu Profesa Kineene wa Mutiso na Daktari T. Olali, kwa kuniongoza tangu mwanzo hadi tamati ya tasnifu hii. Ninatoa shukrani kwani mliniongoza kwa kupitia njia nyingi za kiusomi na kipekee. Baraka nyingi ziwafikie popote mlipo. Vilevile, ningependa kuwashukuru wahadhiri wangu katika idara ya Isimu na Lugha, Chuo kikuu cha Nairobi kwa kuniandaa kiakademia hadi kufikia kuweza kukabili kazi za kitaalamu: Mwenye kiti wa idara, Prof. John Habwe, Dkt. Iribe Mwangi (mratibu), Dkt. Mwenda Mbatiah, Dkt. Jefwa Mweri, Dkt. Zaja Omboga, Dkt. Mbuthia Evans, Dkt. Swaleh Amiri na Mwalimu Mungania B. Ninawaombea Baraka nyingi kwa kazi zenu.

Pia ningependa kutoa shukrani zangu kwa mke wangu Everlyne Awuor Ouma. Umekuwa rafiki wa karibu wa kunielewa na kunishauri, hasa, wakati mambo yangu yalikuwa magumu. Asante sana mwandani wangu na Mungu akubariki.

Isitoshe, ninatoa shukrani zangu kwa watumishi wa Mungu waliosimama nami kwa upendo mlioudhihirisha kwa kuhakikisha kuwa mmesimama nami wakati wa changamoto nyingi zilizonikumba. Kwa kweli bila nyinyi singefika umbali huu nilioufika. Mbarikiwe zaidi.

Shukrani zangu tele ziwaendee wazamili wenzangu tuliojikakamua kutafuta lulu ya masomo. Juliet, Anne, Mary, Ruth, Florence, Merolyne, Moraa, Lily, Motuka, Ogutu, Ndumbu, Keter, Muriithi, Makange, Perllice, Rose, Muniu, Angeline, Grace na Onyonka. Nimeshukuru kwa kuwajua na hata kufanya urafiki nanyi kwa muda huo wote. Mlikuwa wachangamfu hata mambo yalipotulemea kwa changamoto nyingi. Mola azidishe wema wake kwenu.

Ninatoa shukrani zangu zaidi pia kwa wahazili, Esther Ndiege na mwalimu James Ager kwa kuipiga kazi hii chapa kwa bidii na umakini mwingi.

Mwisho, ninatoa shukrani sufufu kwa ndugu zangu na pia marafiki kwa kunipa moyo na kunitia motisha na vilevile kuniombea dua njema wakati wa masomo yangu. Hii ndiyo sababu nimewatungia wote walionifaa utungo huu.

**SHUKRANI NYOTE!**

1. Bismilahi mi naanza,
   Kwa inale Rabana,
   Yeye alo mwongoza,
   Katika yangu kadhiya.
2. Nipate kuwashukuru,
   Mwanzo wangu muhimu,
   Wote walionitukuzu,
   Wahadhiri wa Nairobi chuo
3. Sisahau wasimamizi,
   Wangu hino kazi,
   Maudhui ni ya *Utenzi,*
   *Wa Nabii Isa.*
4. Profesa ni jagina,
   Kineene aitwa jina,
   Kiongozi tasnifu hina,
   Aniongoza vyema sana.

.

5. Wengi waona mwalimu,
Kwangu hata muhimu,
Sio mwalimu mwalimu,
Bali shujaa mahiri.

6. Shujaa wa maandishi,
Yote shairi na tenzi,
Amudu huyu msimamizi,
Kama lugha yake mama.

7. Olali ni Daktari.
Shahada amezikidhi,
Digrii sii tu hadhi,
Bali uwezo wa mtu.

8. Daktari wa kutiba,
Ujinga anatoa tiba,
Nchi ipate makatiba,
Wa maswala ya lugha.

9. Muumba namuombu,
Awachujia mdhalimu,
Wenye roho za sumu,
Kuwafikia vigumu.

10. "Uwaondoshee aduwi,
Ambao hatuwajuwi,
Uwatie na uziwi,
Na pofu kwao.

11. Wape umri mrefu,
Uwajaze uadilifu,
Kuwatondosheya uchafu,
Na mema uwaleteya".

12. Wahadhiri pia wengine,
Wote sio kando pengine,
Bali walikuwa wengine,
Walionipa huu ushindi.

13. Idara kaketi kitini,
Profesa Habwe ni Johni,
Amezama pragmatikini,
Somo mweledi kweli.

14. Ujana nguvu nyingi,
Waratibu sio wengi,
Jina Iribe ni Mwangi,
Daktari wa Fonolojia.

15. Uzamili mehitimu,
Shahada kwenu mekimu,
Kwangu yote muhimu,
Sababu ni nyinyi nyote.

16. Shukrani kwa waumini,
Waliosimama pia nami,
Kwa changamoto nyingi,
Kweli mlinifaa zaidi.

17. Wazamili wenzangu wote,

Wazuri sisi sote,

Shukrani kwenu nyote,

Menifaa zaidi masomoni.

18. Wahazili si wengi,

Majina Esther Ndiege,

Mwingine ni Agere,

James jina jingine.

19. Wengine wa kutajika,

Mke na watoto kushika,

Walinifaa wote hakika,

Mungu awape dua njema.

20. Familia ya baba na mama,

Lugha mlinipa ya mama,

Kiswahili pia nikasimama,

Asanteni nyote mlionifaa.

21. Kalamu mwisho naweka,

Na mafungu kufungika,

Kwa Mola wetu aombeka,

Awatie dua njema.

# IKISIRI

Utafiti huu unahusu uchanganuzi wa maudhui teule katika *Utenzi wa Nabii Isa.* Huu ni utenzi wa miaka ya (1970) lakini una uyakinifu katika jamii ya kisasa kimaudhui.

Kazi hii imegawika katika sura tano. Katika sura ya kwanza tumeshughulikia mambo ya kiutangulizi ambayo yanahusu mada ya utafiti, tatizo la utafiti, madhumuni ya utafiti, sababu za kuchagua mada hii, nadharia tete, upeo na mipaka, msingi wa kinadharia na njia za utafiti. Katika sura ya pili, tumefafanua dhana ya maudhui na baadaye kuangalia baadhi ya mihimili inayotumika kama nguzo dhabiti za maudhui. Mihimili hii ndiyo imeweka msingi wa kukuza zaidi na kuendeleza sura ya tatu kwa kuonyesha msingi wa kukusanya na kuchanganua data ya utafiti wetu.

Sura ya tatu inahusu uchangunuzi wa maudhui teule katika *Utenzi wa Nabii Isa*. Baada ya kuyachanganua maudhui haya katika sura hii. Sura yetu ya nne imejadili jinsi ambavyo maudhui haya yameibua athari katika utenzi wenyewe na vilevile uyakinifu wake katika jamii ya kisasa.

Sura ya tano na ya mwisho ni ya hitimisho la utafiti wetu. Katika sura hii, tumetoa mapendekezo ya utafiti wa kimaudhui zaidi katika *Utenzi wa Nabii Isa.*

## ORODHA YA VIFUPISHO VILIVYOTUMIWA

K.h.j-Kama hapa juu

TUKI-Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili.

Bw - Bwana

Bi - Bibi

Uk - Ukurasa

nw - Na wengine

Prof.- Profesa

Dkt.- Daktari

## YALIYOMO

**Ungamo……………………………………………………………………………… ii**

**Tabaruku…………………………………………………………………………….. iii**

**Shukrani……………………………………………………………………………… iv**

**Ikisiri………………………………………………………………………………….. viii**

**Orodha ya vifupisho vilivyotumiwa………………………………………………… ix**

**Yaliyomo……………………………………………………………………………… x**

**SURA YA KWANZA**

**UTANGULIZI**

**1.0 Utangulizi…………………………………………………………………………… 1**

**1.1 Tatizo la utafiti………………………………………………………………..... 3**

**1.2 Madhumuni ya utafiti……………………………………………………………….. 3**

**1.3 Nadharia tete……………………………………………………………………… 4**

**1.4 Sababu ya kuchagua mada……………………………………………………. 4**

**1.5 Upeo na mipaka…………………………………………………………………… 5**

**1.6 Msingi wa kinadharia….………………………………………………………. 5**

**1.7 Yaliyoandikwa kuhusu mada hii………………………………………………… 8**

**1.8 Njia za utafiti…………………………………………………………………… 11**

**1.9 Hitimisho……………………………………………………………………….. 12**

## SURA YA PILI

## MIHIMILI YA MAUDHUI

**2.0 Utangulizi………………………………………………………………………… 13**

**2.1 Dhana ya maudhui………………………………………………………………. 14**

**2.2 Wahusika……………………………………………………………………… 16**

**2.3 Mandhari………………………………………………………………………… 18**

**2.4 Msuko………………………………………………………………………….. 20**

**2.5 Mtindo…………………………………………………………………………. 22**

**2.6 Sauti ya usimulizi………………………………………………………………. 24**

**2.7 Hitimisho……………………………………………………………………….. 26**

## SURA YA TATU.

## MAUDHUI TEULE KATIKA UTENZI WA NABII ISA.

**3.0 Utangulizi………………………………………………………………………… 27**

**3.1 Ushujaa…………………………………………………………………………… 28**

**3.1.0 Ushujaa wa Nabii Isa………………………………………………………… 29**

**3.1.1 Ushujaa wa Musa…………………………………………………………….. 32**

**3.2 Dini……………………………………………………………………………... 33**

**3.2.0 Nafasi ya Mola katika Dini…………………………………………………… 34**

**3.2.1 Uislamu na Ukafiri……………………………………………………………. 36**

**3.2.2 Sala na Shukrani katika mtalaa wa kidini……………………………………… 38**

**3.3 Miujiza…………………………………………………………………………. 41**

**3.4 Malezi na nafasi ya wanawake…………………………………………………… 43**

**3.5 Sharia za Torati………………………………………………………………… 45**

**3.6 Ndoa……………………………………………………………………………. 46**

**3.7 Maadili………………………………………………………………………………. 47**

**3.8 Dhuluma na Usaliti……………………………………………………………….. 48**

**3.9 Kifo na Ufufukaji……………………………………………………………………. 49**

**3.10 Hitimisho…………………………………………………………………………… 50**

**SURA YA NNE.**

**ATHARI ZINAZOIBULIWA NA MAUDHUI HAYA NA UYAKINIFU WA MAUDHUI HAYA KATIKA JAMII YA KISASA.**

**4.0 Utangulizi…………………………………………………………………… 51**

**4.1 Ushujaa……………………………………………………………………… 52**

**4.2 Dini………………………………………………………………………….. 53**

**4.3 Miujiza………………………………………………………………………. 55**

**4.4 Malezi………………………………………………………………………… 56**

**4.5 Sharia za Torati……………………………………………………………… 57**

**4.6 Ndoa……………………………………………………………………….... 58**

**4.7 Maadili…………………………………………………………………….... 58**

**4.8 Dhuluma na Usaliti……………………………………………………….... 59**

**4.9 Kifo na Ufufukaji………………………………………………………….. 61**

**4.10 Hitimisho…………………………………………………………………. 62**

**SURA YA TANO.**

**HITIMISHO.**

**5.0 Utangulizi………………………………………………………………….. 63**

**5.1 Muhtasari wa Utafiti………………………………………………………… 65**

**5.2 Kuhusu malengo ya Utafiti…………………………………………………. 65**

**5.3 Kuhusu nadharia tete……………………………………………………………….. 66**

**5.4 Mapendekezo ya Utafiti zaidi……………………………………………………….. 67**

**5.5 Hitimisho………………………………………………………………………….. 68**

**MAREJELEO**……………………………………………………………………..69

# SURA YA KWANZA.

# UTANGULIZI

## 1.0 UTANGULIZI.

Utenzi ni ushairi mkongwe katika fasihi ya Kiswahili. Utendi au utenzi ni utungo wenye maudhui yanayosimulia kwa kirefu tukio fulani maalum.

Tuki (2004), inaeleza utenzi kama utungo wa kishairi ulio na beti nyingi ambao huelezea kisa kimoja ama cha kishujaa au tukio la kihistoria na huwa na vina vya kati na kila ubeti huwa na vina vinavyofanana isipokuwa vya mshororo wa mwisho.

Ni bayana kuwa somo la ushairi wa kale halijashughulikiwa vya kutosha kwani katika mihadhara mingi ya kiusomi miswada inayotumika haijachapishwa ili kutumika katika marejeleo. Hata hivyo kuna vitabu vichache vinavyopatikana ambavyo ni vya wataalamu wa kigeni kama Harries (1962), Werner (1932), Knappert (1967) miongoni mwa wengine ambavyo vimeandikwa kwa Kiingereza na lugha zingine za kigeni.

Mhariri wa utenzi huu Abdalla, anadai kuwa *Utenzi wa Nabii Isa* uliandikwa (1977) na mtunzi Musa Mzenga, Almaarufu, Ustadh Shirazi. Ni utenzi unaohusu kisa cha kusisimua cha Nabii Isa, mwanawe Mariyamu aliyezaliwa kimiujiza katika familia ya Bi. Mariyamu. Kuzaliwa kwake kulikuwa kwa kimiujiza kwani alizaliwa na mama Mariyamu bila Mariyamu kuonana kimwili na mume.

Kijumla, utenzi huu ambao ni wa kidini na kihistoria umejikita katika kisa cha kusisimua chenye uhalisia wa kiajabu. Ni kisa kinachohusu maisha ya Mariyamu Binti Imrani ambaye baada ya kuzaliwa katika familia ya Imrani na mamake waliabudu msikitini kila mara,

alichukuliwa na mtume Zakaria aliyeishi naye kwa mafunzo mengi ya kidini na hata kumlea kwa ibada kila mara msikitini. Kabla ya Mariyamu kukutana na mtume wa Mungu aliyemtabiria kuhusu kuzaliwa kwa Nabii Isa na kumvivia nguo na baadaye akapata mimba ya mwana ambaye ndiye Nabii Isa bila kuonana na mume yeyote kimwili.

Nabii Isa alipohitimu umri wa miaka thelathini, alishikilia nafasi ya kuwaongoza wana wa Israeli kama alivyofanya Musa. Hivyo basi, alikamilisha kazi aliyoanza mtume Musa kuwa kiongozi wa kuwaongoza wana wa Israeli kwa uongozi madhubuti, kwani wana wa Israeli walikuwa wamebadili mambo ya sheria na hawakufuata tena, walizidi na uhalifu, walimu na maimamu waliwaonea wanyonge, na wana wa Israeli pia waliunda na kuabudu masanamu.

Mwanzo wa Nabii Isa kuhubiri, mtume huyu wa Ilahi alienda mahekaluni na kuwahimiza watu wa Israeli wasimshabihi Mola, aliwaonyesha heri, upole na mapenzi jinsi alivyojipenda mwenyewe. Alisafiri kwote huku na huku akihubiri, aliamuru mambo mema ya kutenda na kusema na kuwakataza wa Israeli dhidi ya dhuluma na wizi ila kuwajuza mara kwa mara kuhusu Mungu mmoja.

Kisa hiki vilevile kinatuelezea kuhusu miujiza aliyofanya Nabii Isa, kama vile kumwelezea jamaa aliyemsikiza chakula alichokila pamoja na fedha alizonazo mfukoni na katika akiba nyumbani, alimpoza kipofu akaona, kuwaponya wagonjwa, aliunda ndege kutokana na udongo hata wakapaa angani na kutoa sauti na alifufua maiti.

Hata ingawa Nabii Isa alifanya miujiza, wana wa Israeli walihitilafiana iwapo yeye ni Nabii au la. Hili jambo lilileta upinzani mkali miongoni mwao.

Katika utafiti wetu, tutahakiki baadhi ya maudhui katika *Utenzi wa Nabii Isa* kama ushujaa, ndoa, dini, dhuluma na usaliti, miujiza, malezi na nafasi ya wanawake, maadili, sharia za torati, sala na shukrani pamoja na kifo na ufufukaji. Itabainika, kutokana na maudhui haya, kuwa ingawa *Utenzi wa Nabii Isa* umeangazia maudhui kongwe, umebeba uhalisia mwingi wa kiajabu na unahusu jamii ya kisasa, tunatarajia kuwa kwa kuuhakiki utenzi huu kimaudhui, tutakuwa tumeuhuisha hata ingawa ni sehemu ndogo tu ya fasihi ya Kiswahili.

## 1.1 TATIZO LA UTAFITI

Tafiti zetu za tenzi pamoja na uhakiki uliofanywa kwa baadhi ya tenzi unaonyesha wazi kuwa hakuna uhakiki wa *Utenzi wa Nabii Isa* umefanywa kimaudhui isipokuwa yale tumefundishwa darasani katika somo la *Swahili Poetry* katika Chuo kikuu cha Nairobi ili kutosheleza baadhi ya mahitaji ya shahada ya uzamili (M.A).

Abdalla (1976) alihariri *Utenzi wa Nabii Isa*, hata hivyo, maswala ya fani na maudhui hayajashughulikiwa na watafiti na wahakiki wengine kama ilivyo katika tenzi zingine za kidini. Jambo hili limetutia changamoto ya kuhakiki maudhui teule katika *Utenzi wa Nabii Isa* ili kujaza hili pengo lililopo la uhakiki wa utenzi huu kimaudhui na kuangazia maudhui mengine ambayo hayajashughulikiwa katika kazi zingine za kidini zilizohakiki maudhui katika tenzi zingine hapo awali. Hii ndiyo sababu tumehakiki *Utenzi wa Nabii Isa* kimaudhui.

## 1.2 MADHUMUNI YA UTAFITI

Madhumuni yetu hasa katika utafiti huu ni:

a) Kuchanganua kwa kina zaidi maudhui teule katika *Utenzi wa Nabii Isa* ambayo ni pamoja na ushujaa, dini, miujiza, malezi na nafsi ya wanawake, sharia za torati, ndoa , maadili, kifo na ufufukaji na dhuluma na usaliti. Maudhui haya ni teule kwani yanatokana na utenzi huu wa kihistoria, kishujaa na wenye sifa za uhalisia wa kiajabu.

b) Kuthibitisha kuwa binadamu hana uwezo wa kujiamulia hatima yake ya uzazi.

c) Kutathmini nafasi ya majagina katika jamii ya kisasa

d) Kuchunguza baadhi ya mihimili ya kifani inayoendeleza na kujenga maudhui kikamilifu ili kuweka msingi wa kazi hii yetu ya kuhakiki maudhui katika *Utenzi wa Nabii Isa.*

## 1.3 NADHARIA TETE

Utafiti huu wetu umeongozwa na nadharia tete zifuatazo;

a) Mtunzi wa *Utenzi wa Nabii Isa* ameibua maudhui ya ushujaa, ndoa, dini, sharia za Torati, dhuluma na usaliti, maadili, miujiza, malezi na nafasi ya wanawake, pamoja na kifo na ufufukaji

b) Binadamu hana uwezo wa kujiamulia hatima ya kuzaa mwana.

c) Majagina ni mfano mwema wa kuonyesha uhalisia wa kiajabu katika jamii .

d) Maudhui yanajengwa na kuendelezwa kwa mihimili mingi ya kifani.

## 1.4 SABABU YA KUCHAGUA MADA.

Katika utafiti wetu, tumeamua kuchagua mada hii kwa sababu tumegundua kuwa uhakiki wa kimaudhui katika tenzi nyingi za Kiswahili haujaangaziwa vya kutosha na watafiti pamoja na wahakiki katika ushairi wa Kiswahili. Jambo hili humaanisha kuwa mengi kuhusu maudhui hayajashughilikiwa vya kutosha. Hilo ndilo pengo ambalo tunatumai kujaza katika utafiti wetu.

*Utenzi wa Nabii Isa* vilevile haujashughulikiwa kimaudhui. Ni matarajio yetu kuwa mchango huu wetu utawafaa wengi kufanya uhakiki wa kiakademia katika mtalaa wa fasihi kwa kijumla.

## 1.5 UPEO NA MIPAKA

Utafiti huu wetu umejikita katika uhakiki wa maudhui katika *Utenzi wa Nabii Isa* wenye beti 834. Maadamu, kuna mwingiliano mkubwa baina ya maudhui na fani katika utafiti wetu, hatuna budi kuingilia fani kidogo ili kujenga msingi thabiti wa maudhui tunayohakiki. Tumefanya hivyo kwa sababu fani na maudhui huingiliana na fani ndiyo huelekeza maudhui katika kazi yoyote ya fasihi.

Tumejadili baadhi ya nguzo za kuendeleza maudhui ambazo ni wahusika, mandhari, muundo, msuko na usimulizi. Hata hivyo, isisahaulike kuwa lengo kuu la utafiti ni kushughulikia maudhui katika *Utenzi huu wa Nabii Isa*, vilevile, tumerejelea kazi zingine nyingi kama vile tasnifu mbalimbali za wahakiki pamoja na vitabu vya Kiswahili na majarida ya kiusomi ili kufafanua na kuweka utenzi huu katika nafasi yake mwafaka miongoni mwa kazi zingine za kifasihi.

## 1.6 MSINGI WA KINADHARIA

Katika utafiti wetu, mchakato wote huu umeongozwa na nadharia ya uyakinifu wa kijamii katika kuhakiki maswala nyeti. Nadharia hii imetuongoza kama msingi wa kuhakiki maudhui teule katika *Utenzi wa Nabii Isa.*

Mwasisi wa Istilahi "Uyakinifu wa kijamii" alikuwa Stalin (1917). Hata hivyo wasomi wengi pia wameelezea nadharia hii awali na hasa Lukacs (1963). Gorky (1973) pia ameangazia maswala yanayohusiana na nadharia ya Uyakinifu wa kijamii baada ya mwasisi Stalin.

Kwa mujibu wa Lukacs (1963), uyakinifu wa kijamii una uwezo wa kuisawiri jamii katika ukamilifu wake na kuonyesha hatua za jamii hiyo za kimabadiliko.

Lukacs alitoa mawazo mengine kuhusu nadharia hii kuwa Uyakinifu wa kijamii huzingatia hali halisi ya jamii na kuitumia kueleza jinsi jamii inavyoelekea kwenye usoshiolisti.
Brecht, kama anavyonukuliwa na Gatakaa (2012) pia alieleza kuhusu nadharia hii kuwa ni:

*Sanaa ya kimapambano, inayopambana na maoni ya uongo kuhusu hali halisi ya jamii na hisia zinazohujumu maslahi ya binadamu.*

Nadharia hii pia inaangalia hali halisi kutokana na msimamo wa mafalahi na wasomi waliojitolea kuwatetea na wanaopendelea usoshiolisti.

Gatakaa (2012), anadai kuwa, kulingana na Gorky, uyakinifu wa kijamii ni mtazamo wa watu wanaoubadilisha na kuujenga upya ulimwengu.

Mtazamo huu wa Uyakinifu wa kijamii ulihusishwa na mahusiano ya kitabaka katika jamii yaliyozua mikinzano, basi baadhi ya wanafalsafa na wasomi walitafuta njia mbalimbali za kubadilisha na kutafuta suluhisho la machungu hayo. Walitambua kuwa mabadiliko katika jamii hayawezi kutokea iwapo mabadiliko hayatekelezwi katika mfumo wa uzalishaji mali.
Wasomi hawa walifikia maamuzi haya kwa kuwa walitambua mfumo wa uzalishaji mali ndio huamua tabaka la mtu kulingana na nafasi anayoichukua. Kwa mfano, mfumo wa ukapitalisti waonyesha kuwa wanaohidhi mbinu za uzalishaji mali ni mabwenyenye na wanaowafanyia kazi ni mafalahi. Hawa watumizi wao ndio wanaonyongwa na kunyanyaswa na kulipwa mshahara mdogo usiolingana na juhudi zao huku wazalishiwa mali wakizidi kutajirika.

Wanaozalishiwa mali wanapopata faida kutokana na juhudi za wafanyi kazi wao hutumia faida hizo kujistarehesha kwa sababu ya maovu hayo, jamii huwa na mikinzano ambayo itamalizika tu iwapo mfumo wa uzalishaji mali utakapokuwa mikononi mwa mafalahi.

Kutokana na nadharia hii ya Uyakinifu wa kijamii tunaafikiana na Karl Marx (1818-1863) katika nadharia ya umaksi inayoangazia mikinzano inayotokana na tofauti za kitabaka kama anavyoeleza Wamitila (2002) katika kazi yake ya *Uhakiki wa Fasihi*. Vilevile, tunaafiakiana na Gibbe anavyonukuliwa na Gatakaa (2012) kuhusu dhima ya fasihi kuwa fasihi lazima iwe na jukumu la kueleza, kuchambua, kuikosoa na kuiongoza jamii katika lengo lake la kuupindua unyonge na uchafu uliosakini katika jamii hiyo. Iwe na msimamo usiotetereka. Ipinge na kufichua makosa yafanyikayo katika jamii na kushambulia udhaifu wa aina zote katika jamii.

Kwa mujibu wa nadharia hii, wanyonge basi wanahitaji kutiwa ari na motisha ya kuendelea na mapambano yao ya kujikomboa na kujirejeshea utu. Hivyo basi fasihi haina budi kuwapa wanajamii moyo wa kuendelea na mapambano ya kusaka ukombozi. Ndiposa, kazi za fasihi nyingi zinaonyesha sifa bia za vipengele vyote katika maisha ya binadamu wote na katika kazi za kifasihi ili kukomboa jamii dhidi ya hali dhalilishi (Abrahams 1971) kwa mujibu wa Achieng (2012).

Achieng (khj) anafafanua kuwa kufanana kwa maswala haya anuwai huchukuliwa kuakisi seti ya ruwaza bia zilizokuwepo tangu jadi kama inavyoelezwa katika nadharia ya uhakiki wa vikale ya Abrahams (khj). Hii ndiyo sababu binadamu wote ni sawa walipo ingawa kuna tofauti ndogo za kufikirika ambazo husababishwa na tofauti za kimazingira na kihistoria (Mutiso 1999) kwa mujibu wa Achieng (2012).

Wamitila (2002 na 2008), anaeleza kuwa fasihi huwa na sifa bia ambazo huzipa sifa za kiulinganishi. Mhakiki huyu anadai kuwa msingi wa fasihi ni jamii (binadamu) kwa sababu jamii mbalimbali zimeundwa na binadamu. Hii ndiyo sababu kuu ya fasihi kuingiliana.

Mwingiliano wa maswala anuwai katika maisha ya binadamu hutakana na hoja kuwa lugha hutumika kuelezea maswala ya jamii husika ambayo yana sifa zinazoshabihiana. Pili, fasihi zote duniani huchota malighafi yake kutoka kwa jamii na kwa sababu binadamu wote hufanana bila kuzingatia tofauti ndogo za kihistoria na mazingira, basi maudhui yote hufanana kutoka jamii moja hadi nyingine, Japo kila fasihi ni zao la jamii fulani mahususi duniani ambayo hushabihiana. *Utenzi wa Nabii Isa* ni miongoni mwa kazi za kifasihi na basi maudhui yake yameoana sana na maudhui mengine ya kazi zingine za kifasihi. Kwa sababu nadharia ya "Uyakinifu wa kijamii" hutazama uhalisia wa kijamii na mikinzano inayojitokeza katika jamii inayoleta tofauti za kitabaka katika jamii, nadharia hii imetufaa katika kuhakiki maudhui yanayojitokeza katika *Utenzi wa Nabii Isa*. Baadhi ya maudhui hayo ni dini, ushujaa, uislamu na ukafiri, sala, miujiza, ndoa, maadili, dhuluma na malezi na nafasi ya wanawake.

Katika kazi hii, tumetumia nadharia ya Uyakinifu wa kijamii katika kutalii maudhui katika *Utenzi wa Nabii Isa* na kuuweka mahala pake kati ya utunzi wa kijamii. Nadharia hii pia imetumika kuhakiki na kutalii maudhui mbalimbali katika tasnifu yetu. Tumefaulu kufanya hivi kwa kuchunguza jinsi utenzi huu umetumiwa kuihudumia jamii ya wakati huo na sasa.

## 1.7 YALIYOANDIKWA KUHUSU MADA HII.

Utangulizi wetu katika sehemu ya tatizo la utafiti ulionyesha kuwa kulingana na utafiti wetu, hakuna ushahidi tulioupata kuhusu uhakiki wa maudhui katika *Utenzi wa Nabii Isa* ila tu mafunzo tuliyoyapata katika masomo yetu ya *Swahili poetry* katika (MA), Chuo kikuu cha Nairobi.

Hata hivyo, wahakiki wengi wameshughulikia swala la maudhui katika tenzi zingine.

Swaleh (1992) ameshughulikia maudhui katika *Utenzi wa Mwana kupona.* Katika uhakiki wake, alisema kuwa maudhui ya dini yamejikita katika mafundisho ya dini ya kiislamu yanayomtunukia mwanamke nafasi anayostahiki katika jamii yake. Swaleh anaendelea kuwa hadhi anayopewa mwanamke katika jamii yake inamstahiki. Mtafiti huyu anadai kuwa majukumu apewayo mwanamke kwa jamii ndiyo yanachangia kumdhulumu. Kazi ya huyu mhakiki itatufaa kuhakiki maudhui ya dini na nafasi ya Mola katika dini katika jamii.

Wa Mutiso (1985) ameshughulikia swala hili la maudhui, ameangazia maudhui ya Hurafa na uyakinifu katika *Utenzi wa Hamziyya*. Mhakiki huyu katika tasnifu yake ya uzamili, ameshughulikia sifa apewazo Mtume Mohammed (S.A.W) na zile za mashujaa wengine duniani. Kazi yake itatufaa katika kuhakiki maudhui ya ushujaa kama yalivyosawirika katika utenzi huu tunaoshughulikia, *Utenzi wa Nabii Isa.*

Wa Mberia (1989) alihakiki *Utenzi wa Fumo Liyongo* kwa kutathmini sifa za Fumo Liyongo, kama shujaa wa masimulizi. Katika kazi yake, ametupa mwelekeo kuhusu kuhakiki maudhui ya ushujaa katika kazi yetu.

Sifa za kishujaa za Fumo Liyongo zinalandana na za Nabii Isa wa *Utenzi wa Nabii Isa.* Jambo hili linadhihirika kutoka kwa kuyafanya mambo kiuhalisia ajabu hadi anapopata ushindi dhidi ya pingamizi anazokumbana nazo maishani. Jambo tunalolipa pingamizi ni kuwa Wa Mberiah haielezi nadharia aliyoitumia kuhakiki kazi yake.

Mungai (2005) ameshughulikia fani katika *Utenzi wa Mikidadi na Mayasa* ambapo amelinganisha *Utenzi wa Nguvumali* na *Utenzi wa Mikidadi na Mayasa* kifani. Kazi yake hii imetusaidia katika kuhakiki baadhi ya maudhui katika *Utenzi wa Nabii Isa*

Gatakaa (2012) aliangazia uhakiki wa maudhui teule katika *Utenzi wa Mikidadi na Mayasa* aliposhughukia zaidi maudhui ya ushujaa, mahari, dini, vita, umaskini na utajiri. Hata hivyo ni maoni yetu kuwa ingawa watafiti wengine wameangazia maudhui katika tenzi mbalimbali (Khj), swala la uhakiki wa maudhui halijaangaziwa vya kutosha kwani tenzi zingine hazijahakikiwa kimaudhui na *Utenzi wa Nabii Isa* ni miongoni mwa tenzi hizo ambazo hazijahakikiwa. Jambo hili limetutia changamoto ya kuhakiki maudhui teule katika *Utenzi wa Nabii Isa* ili kujaza hili pengo lililopo la uhakiki wa utenzi huu kimaudhui na kiangazia maudhui mengine mengi zaidi ambayo hayakushughulikwa katika kazi zingine za kidini zilizohakiki maudhui katika tenzi zingine hapo awali.

Achieng (2012) pia aliangazia sifa za mashujaa na umuhimu wao kwa jamii zao huku akilinganisha Fumo Liyongo na Lwanda Magere. Katika uhakiki wake aliweza kufafanua sifa za mashujaa wa kijamii na hii kazi yake ilitufaa zaidi katika kufafanua sifa za mashujaa wa kidini na wa kihistoria katika *Utenzi wa Nabii Isa.*

Tofauti na wasomi na wahakiki wenyeji waliozihakiki tenzi na kazi nyingine za kifasihi kimaudhui, kuna wahakiki wengine waliotoa michango yao katika kuzishughulikia na kuzihifadhi tenzi hizi. Hao ni kama vile Knappert (1967), Harries (1962) na kadhalika.

Knappert (1967) alitafsiri baadhi ya beti za *Utenzi wa Tambuka* kwa lugha ya Kiingereza. Utenzi huu umeangazia maudhui na hasa ya dini na ushujaa. Maudhui hayo ni sawa na yanayojitokeza katika *Utenzi wa Nabii Isa* tunaouhakiki kimaudhui. Hivyo basi kazi yake Knappert imetufaa kama marejeleo ya kuhakiki maudhui katika *Utenzi wa Nabii Isa.*

Harries (1962) ameshughulikia maudhui katika *Utenzi wa Al-inkishafi.* Baadhi ya maudhui makuu aliyoyaangazia zaidi ni kama dini, umasikini, utajiri na maangamizi ya binadamu.

Kwa kujikita katika maudhui haya, kazi ya Harries imetufaa katika kuhakiki *Utenzi wa Nabii Isa* kimaudhui.

Kazi tulizotaja hapo juu zimetunufaisha sana kwani tumezirejelea kila mara tukichunguza na kulinganisha dhana ya maudhui katika utenzi wetu. Tunaamini kuwa marejeleo yetu katika tungo yatatupa mwanga katika sehemu nyingi za kazi yetu.

## 1.8 NJIA ZA UTAFITI.

Utafiti wetu huu ni wa kifasihi unaohusu fasihi andishi na hii ndiyo sababu tumefanya kazi nyingi ya kutafiti maktabani.

Tumeusoma *Utenzi wa Nabii Isa* wenye beti 834. Vilevile tumedurusu matini mbalimbali zenye manufaa kwa utafiti wetu kama vile vitabu, tasnifu mbalimbali zilizojadili maudhui na pia majarida na makala yaliyo na mada zinazorejelea tenzi kimaudhui au kijumla.

Pia tumeangalia kazi za awali zilizotumia nadharia ya uyakinifu wa kijamii katika kuhakiki maudhui ili kufanya utafiti wetu kuwa bora zaidi.

Aidha, tumetalii mtandao ili kupata yaliyoandikwa zaidi kuhusu mada yetu ya uhakiki wa kimaudhui.

## 1.9 HITIMISHO

Katika sura hii, tumetoa utangulizi unaohusu uhakiki wa maudhui teule katika *Utenzi wa Nabii Isa*.

Tumetalii mambo ambayo ni ya kiutangulizi ya utafiti huu. Hapa basi tumeshughulikia maswala kama Utangulizi, Tatizo la utafiti, Madhumuni ya utafiti, Sababu ya kuchagua mada, Nadharia tete, Upeo na mipaka, Msingi wa kinadharia wa utafiti na Njia za utafiti.

Sehemu inayofuata ni ya sura ya pili, imehusu ufafanuzi wa dhana ya maudhui pamoja na mihimili yake kwani mihimili hii ya maudhui imeweka misingi ya kuhakiki maudhui katika *Utenzi wa Nabii Isa* kwani maudhui na fani huingiliana.

# SURA YA PILI.

# MIHIMILI YA MAUDHUI.

## 2.0 UTANGULIZI.

Sura hii inahusu ufafanuzi wa dhana ya maudhui. Hapa tumechunguza baadhi ya nguzo za maudhui (mihimili ya maudhui) na kuonyesha uhusiano na mwingiliano wa mihimili hiyo inayojenga maudhui katika Utenzi wetu wa *Nabii Isa.*

Kulingana na Wamitila (2008) kwa mujibu wa Gatakaa (2012 ), Maudhui hayatokei tu katika kazi ya kifasihi bali ni zao la mahusiano na maingiliano ya vipengele na mbinu kadha katika kazi inayohusika. Vipengele hivi vinavyoleta mahusiano na maingiliano ndivyo tunavyovirejelea hapa kama mihimili ya maudhui.

Mdee *nw* (2011), wanadai kuwa mihimili ni boriti au nguzo inayoshikilia dari au paa la nyumba, fremu ya mlango au dirisha, mwimo.

Tunaafikiana na kauli ya Wamitila (khj) kuwa maudhui ni zao la mahusiano na maingiliano ya vipengele na mbinu kadha katika kazi inayohusika. Vilevile, tunaafikiana na kauli ya Mdee *nw* (2011) na kufafanua zaidi kuwa mihimili ni nguzo inayodhamiria kushikilia kitu fulani ili kukisetiri na kuubeba uzito wake.

Kwa hakika, kuna mihimili mingi ya maudhui lakini katika kazi yetu tumechagua ile yenye mahusiano ya karibu sana na mada yetu. Tumejadili maudhui na wahusika, maudhui na mandhari, maudhui na muundo, maudhui na msuko, maudhui na mtindo na maudhui na usimulizi.

Mihimili hii imejadiliwa awali kwa kuwa inaweka msingi thabiti wa mada yetu ya utafiti ambayo ni uchanganuzi wa maudhui katika *Utenzi wa Nabii Isa.*

## 2.1 DHANA YA MAUDHUI.

Kwa mujibu wa Mdee *nw* (2011), Maudhui ni mambo yanayoelezwa katika hadithi, riwaya , hotuba, tamthilia na masimulizi yoyote yale.

Wamitila (2008) anasema kuwa maudhui ni dhana pana inayoweza kuelezwa kwa jinsi mbili ambazo kimsingi zinahusiana. Mwanzo ni kuwa maudhui ni jumla ya maswala au mambo yanayoshughulikiwa katika kazi ya fasihi. Maswala haya ni yale yanayotokana na jinsi mwandishi au mtunzi anavyoikuza mada ambayo ni msingi wa utunzi wa kazi yake.

Jinsi ya pili, Wamitila anayatumia maudhui kukirejelea kiwango cha maana cha matini au kazi ya fasihi.

Mbatiah (2010) anasema kuwa maudhui ni jumla ya masuala yanayoshughulikiwa. Tunaafikiana na kauli hii ya Mbatiah na kusema kuwa maudhui ni maswala makuu yanayojitokeza katika kazi yoyote ya kifasihi na hufafanuliwa kadri ya uwezo wa mwandishi kwa kutumia mihimili yote na kuyaendeleza maswala hayo makuu.

Njogu na Chimerah (1999) wameelezea maudhui kama mawazo ya mtunzi kwa mkabala wa muktadha fulani.

Gatakaa (2012) katika tasnifu yake ya uzamili, anaeleza kuwa maudhui ni ujumbe muhimu unaojitokeza katika kisa kizima katika kazi ya fasihi. Yaani, kile kitu, mtu, sifa ya kibinadamu au hali ya maisha inayozungumziwa hadithini.

Kwa kuegemea fafanuzi za wasomi tulizozitoa kueleza dhana ya maudhui (khj), tunakubaliana na wataalamu na wasomi hawa tuliowataja kuhusiana na maelezo yao kuhusu dhana hii na kusema kuwa maudhui ni mambo, mawazo, fikra kuu au ujumbe muhimu unaojitokeza katika kazi ya kifasihi. Mambo haya yanamulika maisha ya insi kwa jumla katika jamii kama vile utendakazi, mavazi, siasa, ndoa, elimu na uongozi kwa kutaja maswala machache tu. Kila kazi ya kifasihi inazungumzia wazo fulani. Sio rahisi kupata kazi ya kifasihi ambayo haizungumzii jambo fulani. Basi mambo hayo yanayozungumziwa katika kazi ya fasihi ndiyo maudhui.

Tunaamini kuwa katika kazi yoyote ya kifasihi mtunzi anastahili kuafikiana na hali ya maisha ya wanaolengwa katika kazi yake. Hii ni kwa sababu maudhui katika fasihi yanachotwa kutoka kwa hali halisi ya maisha ya jamii lengwa, na kwa sababu mtunzi pia ni mwanajamii, ataandika kuhusu jamii husika kwa kuegemea maisha ya jamii hiyo kisiasa, kiuchumi na kijamii katika wakati maalum wa kihistoria.

Achebe (1975) anaeleza:

> *'Kwangu ni dhahiri ya kuwa mwandishi wa kiafrika anayejaribu kukwepa maswala ya jamii na ya kisiasa katika Afrika ya sasa, ataishia kuandika maandishi yasiyofaa kama mtu anayeacha nyumba ikiteketea ili amkimbize panya anayetoroka moto huo'* (Tafsiri yetu).

Achebe basi anasisitiza umuhimu wa maswala ya jamii kama vile maswala ya kisiasa, kiuchumi na kijamii katika fasihi na tunaafikiana na madai yake.

Mtunzi yeyote basi ana uhuru wa kuteua jambo lolote, bora lichukuane na matarajio yake pamoja na uzoevu wa jamii yake. Akifanya hivyo basi atakuwa amechota malighafi yake (maudhui) kutoka kwa mazingira ya jamii husika.

Wahakiki ni sharti tutambue ujumbe ambao unajitokeza katika kazi nzima tunayoizingatia huku tukitoa mifano ya kuhimili hoja zetu.

## 2.2 MAUDHUI NA WAHUSIKA.

Katika kuendeleza maudhui katika kazi za kifasihi, kuna nguzo zinazoendeleza maudhui hayo kikamilifu. Wahusika ni moja ya mihimili ya maudhui katika fasihi.

Mdee *nw* (2011), Mhusika ni mtu au mnyama katika hadithi anayetenda mambo kadha wa kadha kadiri mtunzi atakavyo ili kujenga hadithi yake . Tunaafikiana na kauli hii.

Wamitila (2010) anasema kuwa wahusika ni viumbe wanaopatikana katika hadithi yoyote ile. viumbe hawa huwa sehemu ya kazi nzima. Pili, wahusika ni binadamu wanaopatikana katika kazi ya kifasihi na ambao wana sifa za kimaadili, kitabia na falsafa ambazo hutambulishwa na wanayoyasema na wanayoyatenda. Wahusika vile vile hutambulishwa kwa maelezo ya wahusika wenzao au msimulizi.

Mbatiah (2010) katika *Mwongozo wa kuhakiki hadithi fupi,* anasema kuwa maudhui ni jumla ya masuala yanayoshughulikiwa katika kazi ya fasihi. Kunaweza kuwa na zaidi ya wazo moja muhimu.

Tunakubaliana na maoni ya wataalamu hawa kuwa wahusika ni viumbe wanaotumiwa na mtunzi katika kujenga na kuendeleza ujumbe kupitia usemi na matendo yao. Wahusika hawa hata hivyo wanaweza kuwa wanyama pia kama alivyosawiri Orwell G (1967) katika riwaya ya *Shamba la wanyama.*
Gatakaa (2012), Wahusika ni viumbe au watendi wanaotumiwa na mtunzi katika kuwasilisha ujumbe kwa hadhira yake. Hutumiwa katika ujenzi na upelekaji mbele wa maudhui.

Kuna aina tofauti za wahusika ambao wanawakilisha watu katika jamii anayoizungumzia mtunzi na hawa wahusika ndio wanaoendeleza maudhui ya mtunzi.

*Utenzi wa Nabii Isa* umesheheni baadhi ya wahusika, wahusika hawa ni wa aina mbili kuu: *Nguli* na *hasidi.*

Mhusika nguli, kwa mujibu wa Gatakaa (2012), ni yule jasiri anayeweza kukabili jambo lolote bila woga au shujaa aliyejitolea kupigana na kutetea haki yake dhidi ya pingamizi nyingi. Katika Utenzi huu wa *Nabii Isa*, hawa nguli ni kama vile Isa, Mariyamu na Mtume aliyepeleka habari ya kuzaliwa kwa Isa, ambao wamejitolea mhanga kupigania haki zao za kijamii. Kutokana nao tunapata maudhui ya mateso, dini, ushujaa, ndoa, malezi na nafasi ya wanawake, miujiza na sharia za torati.

Mhusika hasidi naye ni asiyefurahia mafanikio ya wahusika wengine. Ni mtu mwenye husuda au mkinzani. Katika *Utenzi wa Nabii Isa*, mfano mzuri wa wahusika hasidi ni kama wahabu waliomtesa Nabii Isa na mwanafunzi wa Isa aliyemsaliti. Wahusika hawa tabia zao na matendo yao yameleta mgogoro pamoja na mivutano mikubwa inayokuza maudhui ya ushujaa, dhuluma na usaliti miongoni mwa maudhui mengine katika *Utenzi wa Nabii Isa.* Tunakubaliana na maoni ya wataalamu hawa na kutamatisha kuwa wahusika ni viumbe wa kiubunifu wanaoumbwa na mwandishi na wana sifa zinazotambuliwa kwa wanayoyasema, wanayoyatenda na wanayoyasema wengine kuwahusu.

Hata hivyo, ibainike kuwa hata ingawa maudhui hayawezi kutenganishwa na wahusika, lengo letu kuu sio kuchambua fani na hivyo tumegusia tu wahusika kidogo ili kuuweka msingi wa kuhakiki maudhui katika *Utenzi wa Nabii isa.*

**2.3 MAUDHUI NA MANDHARI.**

Mtunzi anaporejelea mahali panapotendeka jambo fulani pamoja na wakati wa kutendeka kwa tendo hilo basi anarejelea mandhari. Basi mandhari hurejelea mahali na wakati ambapo matukio hutokea katika kazi ya kifasihi.

Tunamwunga mkono Wamitila (2008) anaposema kwamba mandhari ni mazingira ya kimahali, kiwakati na wa kihistoria ambamo kazi fulani ya kifasihi inajikita.

Matukio yanayojitokeza katika kazi yoyote ya kifasihi pamoja na maudhui yanayohusishwa na hayo matukio yanatendeka mahali, wakati na mawanda fulani. Basi ni dhahiri kuwa ili kuchunguza maudhui, mandhari ni msingi muhimu zaidi katika uchanganuzi huo.

Mwandishi huwa huru kuchagua mandhari yake kwa kulingana na ujumbe wake kwa hadhira. Kwa mfano, mwandishi akiwa na lengo la kupasha hadhira yake ujumbe wa umasikini, atachagua mandhari yenye janga lenye miti iliyokauka, nyumba zisizopendeza, watu waliodhoofika kiafya na wanaoonekana wakiwa wamevaa nguo kuukuu na matambara na pia wahusika hawa watachorwa wakiwa na huzuni mwingi. Mandhari haya yatakuwa yasiyovutia kwa hadhira wala kupendeza lakini bado ni mandhari yenye lengo mahususi ya kupitisha maudhui maalum. Katika *Utenzi wa Nabii Isa*, mwandishi ameonyesha shida waliokumbana nazo Nabii Isa na wanafunzi wake, walikumbwa na njaa na maafa ambayo wanamlilia Mtume wa Rahamani awaokoe, wahusika hawa wamechorwa kama wamedhoofika na kuishiwa na nguvu kiasi kwamba hata wanashindwa kutembea (beti 709-7116).

Kama ni ujumbe wa utajiri basi mandhari yatakuwa ya miti mizuri ya kupendeza, nyumba ya kifahari, magari makubwa na ya kifahari yaliyoegeshwa na mengine yanayoendeshwa, barabara nzuri, wahusika wenye afya nzuri na sifa zingine za kiutajiri.

Mazingira yanagawika katika migao mitatu kama vile mgao wa eneo halisi la kijiografia, mgao wa amali za wahusika na desturi zao za maisha yao ya kila siku na vile vile mgao wa wakati ambapo tukio fulani limetendeka na kipindi maalum cha kihistoria au kipindi cha mwaka.

Kuhusu mgao wa eneo halisi la kijiografi, kuna maelezo ya mahali kama vile jinsi chumba kilivyo kwa mfano mandhari ya misikitini palipofanyika mahubiri yakiongozwa na Nabii Isa, nyumbani kwa Mtume Zakaria alipolelewa Mariyamu na kadhalika.

Mgao mwingine ni wa amali za wahusika na desturi za maisha yao  ya kila siku. Katika mgao huu, mambo haya yanadhihirika wazi katika (ubeti 705) ambapo maudhui ya umasikini yameibuliwa kupitia kwa Nabii Isa na wafuasi wake walioshinda njaa jangwani kiasi kwamba hawakuwa na budi kutafuna majani (ubeti 706).

Tatu ni mgao wa wakati ambapo tukio fulani limetendeka, ama kipindi maalum cha kihistoria au kipindi cha mwaka. Kusalitiwa kwa Isa na kuteswa kwake kulikuwa katika wakati fulani na kunazua mandhari yanayodhihirisha maudhui ya dhuluma na usaliti.

**2.4 MSUKO.**

Msuko unarejelea jinsi ambavyo matukio yanafuatana kiusababishi. Pia huitwa ploti. Ni mpangilio wa matukio makuu katika kazi za kifasihi.

Mbatiah (2010), anasema kuwa katika hadithi fupi, elementi kuu ya muundo ni ploti. Kulingana na Mbatiah (khj), Ploti au msuko ni mpangilio wa matukio pamoja na ubainishaji wa vyanzo vyao. Kwake, hivi ni kusema kwamba egemeo la ploti ni matendo ya wahusika na baadhi ya hadithi huwa na ruwaza ya mwanzo, kati na mwisho. Sehemu ya mwanzo inamwingiza msomaji katika mgogoro unaomhusu nguli wa hadithi, sehemu ya kati hukuza mgogoro kwa kuonyesha matendo ya nguli na matokeo yake na sehemu ya mwisho inahusu kusuluhishwa kwa mgogoro.

Tunakubaliana na Njogu  na Chimera (1999) pamoja na Wamitila (2008) na hata Mbatiah (2010) kuhusiana na dhana ya msuko kwa kuwa wameufafanua kama mpangilio wa matukio yanayopatikana katika hadithi na unahusisha matendo ya mhusika mkuu na jinsi yanavyoathiri wahusika wengine katika kazi hiyo ya fasihi .

Msuko ni miongoni mwa dhana za kimsingi katika muundo wa kazi ya kifasihi, jambo hili ni kwa kuwa matendo ya wahusika, vitushi vya wahusika na migogoro kati yao ni msingi muhimu wa maudhui yanayokuzwa katika kazi ya fasihi, hayawezi kutajwa bila ya kuhusishwa na msuko. Migogoro katika kazi ya fasihi hutuelekeza kwenye maswala ya kimaudhui katika kazi hiyo.

Kulingana na Wamitila (2003), misuko ni ya aina nyingi kama: msuko kinzani, msuko msago, msuko mkuu, msuko kioo na msuko rudufu.

Msuko msago ni ule unaoeleza matukio yanayofuatana kwa njia ya moja kwa moja bila ya kutumia mbinu rejeshi. Pia huitwa msuko sahili. Hapa matukio hufuatana kwa njia ya A-B-C-D.

Mtunzi wa *Utenzi wa Nabii Isa,* Musa Mzenga, almaarufu, Ustadh Shirazi ametumia msuko msago kuutunga utenzi huu kwani matukio hapa yanatiririka kwa njia ya moja kwa moja.
Katika utenzi wake wa kidini na kihistoria, kuna kisa cha kusisimua chenye uhalisia wa kiajabu. Kisa hiki kinahusu maisha ya Mariyamu binti Imrani ambaye baada ya kuzaliwa katika familia ya Bwana Imrani na mamake walioabudu msikitini kila mara, kisa hiki kinatuelezea maisha ya Mariyamu kutoka utotoni hadi ujana wake anapochukuliwa na mtume Zakaria aliyeishi naye kwa mafunzo mengi ya kidini na hata kumlea kwa ibada kila mara misikitini kabla ya kukutana na mtume wa mungu aliyemtabiria kuhusu kuzaliwa kwa Nabii Isa. Baadaye Mariyamu aliviviwa guo na mtume na baadaye akapata mimba yake Isa na kumzaa bila kuonana na mume kimwili.

Kurudi kwa Mariamu kwao na mwana kulimbidi amkinge dhidi ya wahasidi kama ilivyo katika jamii nyingi za uswahilini. Hata hivyo, Mariyamu alimlea mwana Isa kwa sharia na kanuni za kidini. Mara nyingi Nabii Isa alipatikana misikitini katika harakati za kupata mafunzo mazuri ya kidini.

Kuhitimu umri wa miaka thelathini kwa Nabii Isa kulimpa nafasi ya kuwaongoza wana wa Israeli kama alivyofanya Musa, hivyo basi alikamilisha kazi aliyoanza Mtume Musa.

Kisa hiki vilevile kinatuelezea miujiza aliyofanya Nabii Isa kwa wana wa Israeli, mbali na miujiza, kisa hiki pia kinatuelezea maisha ya Nabii Isa pamoja na wafuasi wake (wanafunzi). Mahubiri yao na kusalitiwa kwake, na vilevile kufanya mpango wa kumuuwa. Kisa hiki kina mtiririko wa matukio kwa njia ya moja kwa moja, yaani, msuko msago.

**2.5 MAUDHUI NA MTINDO.**

Mtindo ni jinsi ya kutenda jambo, hata hivyo, hakuna njia moja ya kutoa fasili ya neno "mtindo". Jambo hilo limewafanya wataalamu wengi wa fasihi wasiafikiane kuhusu maana ya dhana hii katika uwanja wa fasihi. Wengi wa wataalamu wa fasihi wameonyesha maana ya mtindo kama sawa na fani na ikiwa hivyo basi mtaalamu huyo anaonyesha kuwa mtindo na fani ni kitu kimoja. Nasi tunasema kuwa mtindo ni kipengele kimoja tu cha fani miongoni mwa vipengele vingine vingi.

Kwa mujibu wa Gatakaa (2012), akinukuu Holman:

> *"uchunguzi wa mtindo kwa minajili ya uchanganuzi*
> *unajumuisha kuongezea kwa upekee wa msanii, sifa*
> *ambazo ni za kikawaida kama vile Uteuzi, muundo*

*wa sentensi, tamathali za usemi, wizani, akriri, mshikamano, msisitizo na mpangilio wa mawazo".*

Wamitila (2003) naye anasema kuwa mtindo unarejelea jinsi ya kujieleza katika kazi ya kifasihi. Wamitila anaendelea kusema kuwa uchunguzi wa mtindo unahusisha kuangalia uteuzi wa msamiati, tamathali za usemi, mbinu za balagha, miundo ya sentensi, sura na upana wa aya katika nadhari zake na uakifishaji wake. Anasema kuwa kila mwandishi ana mtindo wake maalum wa kuwasilisha ujumbe katika kazi ya fasihi.

Mbatiah (2010) anasema kuwa mtindo katika fasihi simulizi ni matumizi ya lugha. Hii ni dhana muhimu kulingana na Mbatiah kwa sababu inahusu tofauti iliyopo baina ya fasihi na maandishi ya kawaida

Wataalamu hawa wametoa maoni mazuri. Hata hivyo, ni maoni yetu kuwa mtindo hasa ni mbinu ama njia za kipekee anazozitumia msanii kuwasilisha kazi ya kifasihi. Basi mtindo ni kipengele kikuu cha kuwasilisha maudhui katika kazi yoyote ya fasihi. Matumizi ya lugha katika kazi ya fasihi ni msingi mkuu katika utunzi wa kisanaa na huwa ni nyenzo ya kimsingi anayotumia mwandishi katika utunzi wake. Mbinu tofauti za kimtindo zinaweza kuwa msingi muhimu wa jinsi ya kuwasilisha maudhui teule.

Katika *Utenzi wa Nabii Isa,* mwandishi ametumia mtindo wa kipekee na ndio unaotofautisha kazi yake na kazi nyingine ya mwandishi mwingine.

Ijapokuwa tumetalii mtindo kwa kina, ni vyema ijulikane kuwa swala letu la utafiti linahusu uhakiki wa maudhui teule katika *Utenzi wa Nabii Isa*, jambo ambalo tumelizungumzia kwa

kina katika sura ya tatu, maelezo ya mtindo hapa basi kwa kiasi kikubwa tu ni ya kuweka msingi wa kuhakiki maudhui yanayojitokeza katika utenzi huu.

## 2.6 SAUTI YA USIMULIZI NA MBINU ZA USIMULIZI.

Usimulizi ni sauti zinazosimulia hadithi katika kazi ya kifasihi. Sauti hizi huweza kuwa katika nafsi ya kwanza, ya pili au ya tatu. Sauti ina umuhimu sana katika kazi ya kifasihi kwa kuwa huweza kuathiri dhamira, mwelekeo, maudhui na mtazamo wa msanii kuhusu maswala jadiliwa.

Wamitila (2003) anaeleza usimulizi kama jinsi ya kueleza matukio katika hadithi. Anasema kwamba katika kazi yoyote ya kifasihi, huwa mna kisa au hadithi fulani ambayo husimuliwa na msimulizi, msimulizi huyo husimulia hadithi yake kwa mtindo fulani na kwa njia maalum.

Usimulizi ni nguzo kuu katika uwasilishaji wa matukio katika kazi za kifasihi kwa kuwa wahusika na matendo hayawezi kuwafikia wasomaji bila usimulizi. Sauti ya msimulizi inapotokea huelekeza maudhui.

Usimulizi wa nafsi ya kwanza hutambulishwa na matumizi ya kiwakilishi “mimi”. Msimulizi wa nafsi ya kwanza huweza kuwa mshiriki katika matukio yaliyopo katika kazi ya kifasihi au anayeshuhudia tu (Wamitila 2002). Na athari ya usimulizi wa nafsi ya kwanza ni kuwa inarahisisha ushawishi wa msimulizi kwa hadhira yake na vile vile usimulizi huo huwezesha hadhira kuwa karibu na mawazo pamoja na ulimwengu wa msimulizi.

Usimulizi maizi (wa nafsi ya tatu) kulingana na wamitila (2002) ni usimulizi unaofuata mkondo unaodhihirisha ufahamu wa siri wa mambo yote. Msimulizi maizi hutambuliwa kwa

mofu “a”. Aina hii ya usimulizi ina sifa za kiunguungu za kikielewa kila kitu kinachowahusu wahusika, mandhari, mwelekeo na saikolojia ya viumbe wa hadithini. Usimulizi huu humpa msanii uhuru wa kuchagua atakayoyasema kuhusu wahusika wake.

Katika *Utenzi wa Nabii Isa*, mwandishi amechanganya nafsi ya tatu pamoja na nafsi ya kwanza, lakini kwa kiwango kikubwa, utenzi huu umesimuliwa kwa nafsi ya tatu. Kwa mfano, maelezo yanayotolewa na mwandishi katika sehemu ya pili wakati Mariyamu alikuwa apatiwe mtu wa kumlea yametolewa kwa nafsi ya tatu.

Babake akatafuta,
Mtu yeyote kupata,
Mwanawe kumpakata,
Malezi kumfanyia (ubeti 56).

Kuhusu miujiza ya Nabii Isa, maelezo ya jinsi Isa alivyoazimia kuunda ndege na akaweza kupaa yamesimuliwa kwa nafsi ya kwanza kwani Nabii aliweza kusawiriwa akizungumza moja kwa moja na wale waisraeli. kwa mfano,

Akawambia sikiza,
Ambayo nawaeleza,
Sasa nitatengeneza,
Ndege na kuwarushia (ubeti 452).

## 2.7 HITIMISHO.

Sura hii imehusu ufasili wa dhana ya maudhui. Pia tumejadili baadhi ya mihimili ya maudhui. Tumejadili mihimili hiyo kwa sababu ndiyo nguzo ambazo kwazo maudhui hujengwa na kuendelezwa katika kazi yoyote ya kifasihi. Hata hivyo mihimili hii ni mingi zaidi na ikawa hatuna budi kuchanganua michache inayoafikiana na mada yetu ili kuweka msingi dhabiti wa kuhakiki maudhui katika *Utenzi wa Nabii Isa.*

Katika uchanganuzi wa mwingiliano wa mihimili hii na maudhui, tumewanukuu baadhi ya wataalamu na maoni yao kuhusu mihimili hii inavyojenga na kuendeleza maudhui. Pia tumetoa mathibitisho kutoka kwa *Utenzi wa Nabii Isa* tunaouhakiki.

Hata ingawa tumechanganua mihimili hii ya maudhui, ni vyema ifahamike kuwa utafiti wetu hasa unahusu uhakiki wa maudhui teule katika *Utenzi wa Nabii Isa.*

# SURA YA TATU.

## MAUDHUI TEULE KATIKA UTENZI WA NABII ISA.

### 3.0 UTANGULIZI.

Hii ni sura muhimu kwani ndipo tumechanganua *Utenzi wa Nabii Isa* kimaudhui na huu uchanganuzi ndio swala letu kuu la utafiti wetu. Hivyo, basi ni bayana kuwa hiki ndicho kiini cha utafiti wetu.

Kabla ya kuchanganua maudhui hayo, tumetoa fasili ya baadhi ya istilahi zinazohusiana na mada yetu na baadaye tukachunguza jinsi mtunzi alivyojenga maudhui ya ushujaa, dini, miujiza, malezi, sharia za torati, ndoa, maadili na dhuluma na usaliti pamoja na kifo na ufufukaji katika utungo wake, hasa tumezingatia hoja ya kuwa dini ni asasi muhimu katika uendelezaji wa maudhui mengine katika utenzi huu.

“Uhakiki” ni hali ya kudhibitisha ukweli wa jambo fulani**.** Kulingana na Mdee *nw* (2011), uhakiki ni hali ya kudhibitisha iwapo jambo au tendo fulani ni la kweli, uthibitishaji. Ni sawa na uhakika au hali ya kujua ukweli.

“Teule” ina maana ya kuchagua kitu au jambo ili kuliidhinisha kufanya kazi. Ni iliyochaguliwa lakini kabla ya kupishwa na kufanya kazi, hutokana na teua, kiteuzi chenye maana ya kuchukua kitu kimoja kizuri na kinachofaa kati ya vitu vingi (Mdee *nw* 2011).

Tunakubaliana na maoni haya ya Mdee *nw* (2011) na kufafanua zaidi kuwa uhakiki wa maudhui teule katika *Utenzi wa Nabii Isa* ni uchanganuzi au uchambuzi wa baadhi ya maswala yaliyochaguliwa kutokana na maswala ibuka katika *Utenzi wa Nabii Isa* na

uchaguzi huo pia umezingatia msingi wetu wa kinadharia ambao ni kigezo chetu cha kuhakiki maswala haya. Miongoni mwa maswala hayo ni yaliyojadiliwa hapa.

### 3.1 USHUJAA.

Mdee *nw* (2011), ushujaa ni hali ya kuwa na moyo wa ujasiri. Hali ya kutokuwa na woga, ujasiri au uhodari.

Tunakubaliana na madai haya na kufafanua ushujaa kama hali ya kuwa na moyo wa kukabiliana na jambo au hali yoyote inayozuia mafanikio bila kuwa na woga.

Malinowski kwa mujibu wa Gatakaa (2012), anaeleza kuwa mahitaji mengi katika jamii huibua taasisi mbalimbali na mojawapo ikiwa ni taasisi ya ushujaa.

Kwa mujibu wa Gatakaa (2012), taasisi hii ni muhimu sana katika kusawazisha hali zilizoenda mrange katika mfumo wa jamii. Kauli hii ya Malinowski (khj) ni ya kweli kwa sababu ushujaa ni wa maana sana kwa binadamu katika shughuli za ukombozi dhidi ya hali dhalilishi za kuzorotesha kiuchumi, kisiasa, na kijamii.

Hali ya ushujaa inatokea pale ambapo kuna mtu ambaye ni shujaa au jagina. Kuzuka kwa ushujaa ni kwa hali, kipindi na mazingira maalum ya kijamii.

Kulingana na Gaster, anavyonukuliwa na Mungai (2005), jagina ni mtu ambaye humiliki uwezo zaidi kuliko uwezo wa watu wa kawaida na hutumia uwezo huu kiujasiri na huwa tayari kuyahatarisha maisha yake kwa manufaa ya watu wengine.

Kulingana na Tuki (2004), shujaa ni mtu mwenye moyo thabiti anayeweza kukabili mambo, hata kama ni hatari, jasiri, nguli, jogoo, jabali, abtali, ghazi, nyamaume.

Kwa jumla, tunaunga mkono maoni ya wataalamu hawa na kufafanua shujaa kama kiumbe aliye na sifa za kiajabu anayekuzwa na wanajamii na pia kujikuza mwenyewe ili ajinufaishe na kunufaisha watu wengine.

Maelezo ya Chiraghdin, Nabhany na Buruwa kwa mujibu wa Gatakaa (2012) kuwa maudhui ya tenzi katika fasihi mbalimbali za ulimwengu huwa ni ya kuwatukuza watu waliotenda vitendo vikubwa (mashujaa) katika historia zao ni ya kweli kwa sababu mtunzi Musa Mzenga amefanya hivyo kwa kuwatukuza mashujaa kama Nabii Isa na Musa kama mashujaa wa kidini, kijamii na wa kihistoria.

Katika uhakiki wa maudhui ya ushujaa, tumetalii ushujaa wa Nabii Isa mwanzo, kisha baadaye tuhakiki ushujaa wa Musa kama walivyosawiriwa katika utenzi huu.

**3.1.0 USHUJAA WA NABII ISA.**

Nabii Isa ni mhusika mkuu aliyesawiriwa kama shujaa aliyetoka katika familia ya Bi. Mariyamu kighafla bila kukutana kwa mume na muke kimwili. Mhusika huyu ameonyeshwa kama shujaa kutoka mwanzo hadi mwisho wa utenzi huu. Ushujaa huu tunaulinganisha na ule wa Fumo Liyongo, shujaa wa kimasimulizi kama anavyosema Wa Mberia (1989) na Achieng (2012) aliyemtazama Fumo Liyongo kama shujaa wa kijamii.

Mtunzi amemtanguliza mhusika huyu akiwa bado hajazaliwa. Kule kuzaliwa kwake, kulelewa kwake katika mafunzo ya kidini hadi maisha yake akiwa mhubiri miskitini na hata matendo yake ya kimiujiza yanamtambua kama shujaa halisi wa kidini, kijamii na kihistoria.

Kuingiliana kwake na dini ya kiislamu kuna kigezo kikuu katika ushujaa wake kwani aliweza kutenda mambo kishujaa, hoja hii inadhibitisha kuwa dini ni asasi muhimu ya kuendeleza maudhui ya ushujaa.

Asasi ya dini imefaulisha mwendelezo wa ushujaa wa Nabii Isa kwani ushujaa wake ulionekana kutoka kuzaliwa kwake hadi katika matendo yake ya kimiujiza yaliyoonyesha sifa sufufu za kijagina.

Kwa kurejelea sifa za majagina kama anavyoeleza Wa Mberia (1989) na vile vile Achieng (2012), majagina wanatambuliwa kwa sifa zao za kiuhalisia ajabu kwani kuzaliwa kwao hutabiriwa, majagina hupewa majina mengi, kabla ya kuzaliwa kwao kunakuwa na msukosuko katika jamii, ujana wao hauelezwi sana, huwa wana maadui wengi, wanasalitiwa na pia kufa kwao sio kwa magonjwa bali ni kwa kupenda kwao. Madai haya ya Wa Mberia yanadhihirika katika *Utenzi wa Nabii Isa* kwani baada ya Mariyamu kukutana na mtume aliyemtabiria kuzaliwa kwa Nabii Isa, Mariyamu alipata mimba bila kuonana na mume kimwili baada ya mtume kumvivia nguo na akapata mimba ya mwana, Nabii Isa.

Isa pia alipewa majina mengi kama Rasuli (ubeti 792), Rasili, Mtume (ubeti 347). Sifa hizi zinamtambua Nabii Isa kama Shujaa halisi wa kihistoria, kijamii na kidini.

Kuhusu huu ushujaa wa Nabii Isa, alitenda mambo mengi kimiujiza kama vile kumweleza yule jamaa aliyemsikiliza kuhusu chakula alichokila pamoja na fedha alizo nazo mfukoni na hata mabaki ya fedha hizo alizo nazo katika akiba nyumbani.

Isa pia alimpoza kipofu na huyo kipofu akaweza kuona, aliwaponya wagonjwa na kufufua maiti, kuunda ndege kwa kufinyanga udongo na hao ndege wakapaa angani na kutoa sauti.

Pia kuzaliwa kwa Nabii Isa kulikuwa kiajabu kwani alizaliwa bila kukutana kwa mume na mke kimwili (ubeti 147) bali Bi. Mariyamu aliviviwa nguo na mtume aliyetumwa na Mola na akapata mimba ya Nabii Isa. Miujiza hii yote inajitokeza kwa imani ya Nabii Isa na Bi. Mariyamu pamoja na wanajamii hii katika dini ya kiislamu. Hivyo basi imani ya kidini ni muhimu kwani husaidia kuendeleza maudhui katika kazi za kifasihi.

Madai haya yetu kuhusu Nabii Isa kuwa shujaa yamelandana na madai ya Achieng (2012) kuhusu sifa za mashujaa hasa akirejelea Fumo Liyongo na kumlinganisha na Lwanda Magere. Achieng anaeleza sifa sufufu za majagina wa kihistoria na kusema kuwa mashujaa huzuka kutatua mahitaji fulani, kuzaliwa kwa mashujaa hutabiriwa, utoto na ujana wa mashujaa hauelezwi, cheo cha shujaa hakipatikani kwa urahisi, shujaa ana maadui wengi, shujaa huwa na akili pevu, mara nyingi shujaa husafiri, maisha ya shujaa yamejaa dhiki, maisha na matendo ya mashujaa ni ya kimiujiza, mashujaa hawaeleweki kwa uwazi, kitu kizuri kinahusishwa na shujaa na mashujaa aghalabu "hawafi" na wakifa hukumbukwa milele.

### 3.1.1 USHUJAA WA MUSA

Kwa kupitia mhusika msaidizi mtume Musa, mtunzi ametusawiria maudhui ya ushujaa hasa katika maelezo kuwa mtume Musa alikuwa kiongozi madhubuti (beti 300-302) aliyeongoza waisraeli na katika uongozi huo wake aliongoza umati kwa kufuata taurati alizopewa na Mungu hata ingawa wana wa Israeli baadaye waliasi uongozi wake na kuanza kuabudu masanamu na kulipisha wanyonge ushuru ulio wa juu ilhali viongozi hawakulipishwa (beti 9-16).

Mtunzi anaeleza kuwa wana wa Israeli walikuwa wamebadili mambo ya sharia na hawakufuata tena, walizidi uhalifu, walimu na maimamu waliwaonea wanyonge kwa kuwalipisha ushuru mwingi ilhali wenyewe hawakulipa, wana wa Israeli pia waliunda na kuabudu masanamu. Hoja hii inaoana na maoni ya Karl Marx (1818-1883) na Marx Weber (1864-1920) kuhusu nadharia ya mikinzano katika jamii (Uyakinifu wa kijamii).

Hata hivyo, ushujaa wa Mtume Musa ndio ulioweka msingi wa uongozi madhubuti wa Nabii Isa kwani Isa aliendeleza tu aliyoyaanza Musa katika uongozi wa Israeli (beti 301-302).

> ‘Uongozi madhubuti,
> Wa kuongoza umati,
> Shikilia taurati,’
> Ya Musa kuirudia (ubeti 301).
>
> ‘Maongozi yayo hayo,
> Wewe endelea nayo,

Iwe na makusudiyo,

Watu wako kufunzia (ubeti 302).

Katika beti hizi, Mungu anamwamuru Nabii Isa kuwa achukue uongozi aliofanya mtume Musa kwa wana wa Israeli na azirudie sheria za taurati ili washike vizuri na aendeleze uongozi huo madhubuti.

Kuhusu miujiza, Musa alikuwa mtume wa kwanza kufanya miujiza kama vile kugeuza fimbo lake kuwa nyoka mbele ya wazee wakishuhudia (ubeti 358). Hii ni ithibati kuwa hata miujiza aliyofanya Nabii Isa ilianza na mtume Musa.

**3.2 DINI.**

Dini ni kama imani inayohusiana na kuwepo kwa Mungu au miungu. (Mdee nw 2011).

Tuki (2004), wamefafanua dini kama imani inayohusiana na mambo ya kiroho, kwamba kuna muumba ambaye aliumba ulimwengu huu na kwamba ndiye mtawala wa kila kilichomo. Pia ni mfumo fulani wa imani na njia ya kuabudu, kusali na kuheshimu / kutii huyo muumba kama vile Ukristo, Uislamu au Ubudha.

Tunakubaliana na maoni haya na kufafanua dini kama uhusiano wa kiroho unaohusu imani kubwa baina ya wanadamu na Mungu.

Imani ya kidini inashikilia kuwa Mungu aliumba ulimwengu na hata binadamu ambaye hata baada ya kuaga inaaminika kuwa roho yake inaishi.

Katika *Utenzi wa Nabii Isa*, dini inayorejelewa hapa ni ya uislamu.

### 3.2.0 NAFASI YA MOLA KATIKA DINI.

Katika asasi ya dini, kuna imani kuu kuhusu Mola. Hasa katika mtalaa wetu huu, tumeshughulikia nafasi ya Mola katika dini ya kiislamu.

Mwandishi Mzenga (1977) ameonyesha kuwa katika dini ya kiislamu Mungu ni mmoja tu (ubeti 347) na uwezo wake umesifiwa kutoka mwanzo hadi mwisho. Huyu ndiye anayeabudiwa hata ingawa haonekani (beti 348-355), na waisraeli wanalalamika kuwa hawawezi kumwabudu anayewatuma mitume hasa Musa na Isa naye Mungu mwenyewe haonekani.

Katika beti za mwanzo, mtunzi amejiweka mkononi mwa Mola ili amwongoze apate kufaulu katika utunzi wake na akaendelea kuwakashifu wasiomjua Mola na kuabudu masanamu (ubeti 10).

Mtunzi vile vile ameeleza kuhusu waliomcha Mungu kama vile Musa alivyowafunza wana wa Israeli mambo mengi mazuri (ubeti 12) kwa kufuata sharia za taurati hata ingawa baadaye wana wa Israeli waliasi mafunzo yake.

Wengine waliomcha Mungu ni kama vile Bwana Imrani na mkewe waliokesha mara kwa mara wakiwa katika sala misikitini (beti 18-21).

Katika mahubiri ya Nabii Isa, aliwaonya waisraili dhidi ya ibada za kuabudu sanamu na kuwa wanapaswa kuamini katika Mola pekee (ubeti 633).

> Akawa kuwakabili,
>
> Wenziwe wa"siraili,
>
> Waachane na batili,

Sanamu kuzihunia (ubeti 633).

Kwa jumla, Imani katika dini ya kiislamu inaweka wazi kuwa Mungu ni mmoja ambaye anafaa kuabudiwa katika hali zote; katika hali ya shida na hata katika mafanikio.

Wa Mberia (1989) amerejelea sifa za majagina kama wenye majina mengi, jambo hili limeonekana katika *Utenzi wa Nabii Isa*. Tunakubaliana na maoni ya Mberia (khj) kwani mungu huyu ni shujaa wa kidini mwenye majina mengi kama Ela  (ubeti 615 ), Jalia (beti 98-99), Karimu (ubeti 595), Rabana (ubeti 119), Ilali (ubeti 320) kama anavyorejelewa katika *Utenzi wa Nabii Isa*.

Katika muktadha wa dini, Mungu pia amesawiriwa kama asiyeshindwa na jambo. Mjumbe wa Mungu anaeleza kwa Mariyamu kuwa Mungu ni yule asiyeshindwa. Hii ni kwa sababu Mungu aliwezesha Mariamu kuzaa mwana bila kuonana na mume kimwili.
Mungu tena amesawiriwa kama mwenye uwezo mkubwa zaidi kwani aliumba binadamu kama vile Isa bila baba kudhubutu (ubeti 588).

Na hili kwa Mola wetu,
Si kazi kuumba mtu,
Pasi baba kudhubutu,
Ndivyo Isa metukia (ubeti 588).

Katika *Utenzi wa Nabii Isa,* Mola vilevile ameonyeshwa kuwa mkarimu kwa sababu alijalia mtume Zakaria na akapewa nafasi ya kumlea Mariyamu baada ya kupewa kwa kura nyingi zaidi miongoni mwa wote waliogombea kupata nafasi ya kumlea (Beti 78, 81).

Pia ameonyeshwa kuwa ni mwenye rehema kwa sababu Mariyamu alimwomba amwepushie dua ya hifadhi njema.

### 3.2.1 UISLAMU NA UKAFIRI.

Uislamu ni imani katika dini inayoshikilia kuwa Mungu anayeabudiwa ni mmoja tu na kwamba mjumbe wa kipekee wa dini hii ni Mtume Mohammad (S.A.W) ilhali ukafiri kwa upande mwingine ni ule moyo wa kutoamini katika dini ya kiislamu na kufanya matendo yanayokinzana na matakwa ya dini hii.

Kulingana na Tuki (2004), Uislamu ni dini inayofuata imani ya kuwa Mungu anayepasa kuabudiwa kwa haki ni mmoja tu na kwamba Mtume Mohammad (S.A.W) ni mjumbe wake.

Mdee *nw* (2011), uislamu ni dini ambayo msingi wake ni Kurani Takatifu na inayofuata imani ya kuwa Mungu anayepasa kuabudiwa ni mmoja tu na kwamba mtume Muhammad (S.A.W) ni mjumbe wake wa mwisho.

Tunakubaliana na maoni ya wataalamu hawa na kufafanua zaidi kuwa imani hii ya kidini ni ya kiroho na katika uislamu kuna imani inayoshikilia kuwa mungu ni mmoja tu na mtume Mohammad ndiye mjumbe wa mwisho asiyepimwa na mwingine katika dini hii.

*Utenzi wa Nabii Isa* ni utenzi ambao umeegemea dini ya kiislamu kwa kiwango kikubwa zaidi. Utenzi huu unahusu kisa cha Mungu kumleta Nabii Isa miongoni mwa wana Israeli ili awaeleze kuhusu sharia za taurati walizopewa na mtume Musa (ubeti 41). Mungu alimleta Nabii Isa kwa kuwa wana wa Israeli walikuwa wakiabudu masanamu na kuwafanya kuwa miungu wao (ubeti 10)

Katika utenzi huu, msanii amesawiri wahusika wachache ambao wameshikilia imani katika dini ya uislamu ipasavyo kama mtume Zakaria na mkewe, Bwana Imrani na mkewe na vile vile wahusika wengine kama vile mitume waliopeleka ujumbe wa Mungu asiyeonekana kamwe (beti 112-122).

Mariyamu pia alishikilia Imani katika dini ya uislamu kiasi kwamba alipokuwa kwao kwa Bwana Imrani alisali misikitini mara kwa mara alipopata mafunzo mazuri, hili aliliendeleza hata alipoenda kwa Zakaria.

Nabii Isa vilevile ameumbwa na mwandishi katika utenzi huu akiwa na imani katika dini, alihubiri na kutenda miujiza kwa uwezo wa Mungu (beti 320-527).

Waumini wote wa kiislamu wamesawiriwa katika utenzi huu kama watu waliomtegemea Mungu wao kwa mambo yote na wanatambua kuwa Mungu ndiye mwenye majibu yote.
Katika harakati za kupata mlezi wa Binti Mariyamu, watu wote waliamini kuwa Mungu ndiye achaguaye mlezi (ubeti 51).

Waislamu pia wameamini kuwa wao wote ni ndugu katika sharia na imani ya dini (Ubeti 68) na hawana mapendeleo yoyote wala ubaguzi wowote kwa yeyote. Jambo hili linajitokeza kinyume na wale ambao ni makafiri walioabudu masanamu.

Kwa waumini wa dini ya Uislamu, japo maagizo ya Mungu yanaonekana kuwa ni magumu, ni sharti yatimizwe na hii ndiyo sababu Mariyamu mwana wa Imrani anatii maagizo ya Mungu kupitia kwa mjumbe baada ya kuthibitisha kuwa alikuwa kweli ni mjumbe mtume wa

Mungu (ubeti 169). Mariyamu alikubali amri zake mtume na akaviviwa nguo, hatimaye Mariyamu akapata mimba ya Nabii Isa.

Binti Mariyamu alipozaa mwana Isa bila ndoa, wengi walimdhania kuwa mwenye dhambi lakini baadaye Nabii Isa amwondoa lawama kwa kueleza kuzaliwa kwake (beti 244, 247, 249, 265). Isa anaeleza jinsi alivyotumwa na Mola kueleza kuhusu kuswali, kufunga na hata heshima kwa mama (beti 266-277), haya maneno ya Nabii Isa yalikuwa ni kuhusu baadhi ya mihimili iliyoshikiliwa katika uislamu.

Kuhusu ibada, Inabainika kuwa hata ingawa Isa alichukua muda mwingi msikitini katika ibada (beti 289, 299), wengi bado hawakuacha kutenda maovu na kila asubuhi hao walitafuta njia ya kuhalalisha ibada haramu ya kuabudu masanamu (ubeti 310).

### 3.2.2 SALA NA SHUKRANI KATIKA MTALAA (ASASI) YA KIDINI.

Kulingana na Mdee *nw* (2011), sala ni dua zinazotolewa kwa mwenyezi Mungu kwa lengo la kumshukuru au kumwomba atusaidie.

Tuki (2004), wanafafanua sala kama maombi kwa mwenyezi Mungu; dua au shughuli za kumshukuru Mungu.

Madai ya wataalamu hawa kuhusu sala ni ya kweli kwani sala inahusiana hasa na dua za kumshukuru na kumwomba mwenyezi Mungu usaidizi wowote. Hivyo basi, tunakubaliana na maoni ya wataalamu hawa.

Katika dini ya kiislamu, sala ina nafasi muhimu sana katika jamii hii. Mambo mengi yanayotukia kwa wafuasi wa dini hii yanafanyika kwa kujibiwa kwa sala. Maombi ya Bwana Imrani na mkewe walipozidi kumwomba Mola awajalie mwana na hasa wa kiume yanajibiwa. Mungu anapojibu maombi yao, anawapa mwana wa kike (Mariyamu) (ubeti 40) kwa kuwa Imrani na mkewe walimtumikia Mola kwa nyoyo zao (beti 17, 27, 28, 29, 32).
Mke wa Imrani kwa upande wake alimpa Mola shukrani za dhati kwa kumpa mtoto hata ingawa alitarajia mtoto wa kiume akapewa wa kike (beti 40-44). Hii inaonyesha kuwa jamii hii inathamini shukrani kwa chochote wapatacho.

Mwandishi wa *Utenzi wa Nabii Isa* amemsawiri Mola kama mwenye rehema kwa kuwa anawarehemu waumini wa dini ya kiislamu au hata makafiri bila kubagua na hii ndiyo sababu hata mamake Mariyamu pia alipomwomba amwepushie shetani, alimfaidi.
Mola amesawiriwa kama anayetegemewa kwa mambo yote hata katika kutoa uamuzi wa atakayemlea Mariyamu, kura hizo wanazipiga kwa imani kuwa matokeo yake ni kwa mapenzi ya Mola (ubeti 83).

Kwenda kwa Bibi Mariyamu safarini kule mashariki kulikuwa na jambo, alishikwa na woga alipomwona ghulamu njiani akiwa na hofu kuwa asije akamtendea maovu. Papo hapo basi bibiye akaamua kutoa dua zake kwa Mola ili amhifadhi na kumwepushia shari (beti 122, 118-119)

Mbele macho kiyafuma,
Akamuona ghulama,
Njiani amesimama,
    Uso nuru huawa (ubeti 112).

Taa wudhu akasoma,
Dua ya hifadha njema,
Ila Mola wa rehema,
  Shari kumwepushia (ubeti 118).

Akaomba ya Rabbana,
Muumba mtajikana,
Nikinga na wenye lana,
  Wasiwe kunandamia (ubeti 119).

Imani katika ibada inaonekana zaidi baada ya Mariyamu kukutana na mtume na kumvivia nguo na hatimaye Mariyamu kupata mimba, tunaelezwa kuwa hakupunguza ibada, aliendelea kusali (beti 178-179) na hata kutembelewa na malaika waliomletea vyakula na vinywaji (beti 182-185).

Nabii Isa vilevile alishiriki katika ibada kutoka utotoni na kushikilia mafunzo ya dini misikitini. Pia hakupoteza wakati michezoni (ubeti 282).

Katika kuhubiri kwake, Nabii Isa alitenda miujiza ambayo kabla ya kuitenda angemtolea Mungu dua zake. Mwanzo miujiza yake inaonekana pale alipowafufua watu (beti 506-517). Wale walioona miujiza yake Nabii Isa waliabudu Mungu (ubeti 526).

Kuhusu sala, wafuasi wa Nabii Isa walipokosa chakula katika msimu wa kiangazi, walihangaika zaidi na wakakosa la kufanya lakini Nabii Isa alipoinua macho juu kwa sala,

Mola alimjibu kwa kuwapa vyakula; chakula chenyewe kikiwa ni maida ambayo yalikuwa matamu yasivyomithilika, hapo basi walimshukuru Mola kwa kuwajalia (beti 746-761).

**3.3 MIUJIZA.**

Mdee *nw* (2011), Muujiza ni jambo la ajabu; kioja, shali, nduli au dungudungu.

Kulingana na Tuki (2004), muujiza ni jambo lisilokuwa la kawaida; shali, ajabu, kioja au dungudungu.

Madai ya wataalamu hawa ni ya kweli kwani nasi pia tunafafanua muujiza kama jambo la ajabu ambalo sio la kawaida kutendeka.

Katika *Utenzi wa Nabii Isa*, baadhi ya matendo ya Nabii Isa yamefanya utenzi huu kupata sifa za kiuhalisia ajabu.

Kwa mujibu wa Wamitila (2003:274). Uhalisia ajabu ni dhana iliyobuniwa na msanii wa ujerumani Franz Roh inayohusishwa na sifa mbalimbali za kuyaelezea matukio ya kifantasia au ya kiajabu au kichawi kwa namna ya moja kwa moja kwa namna inayoyafanya yaonekane kama ya kawaida na mpaka uliopo kati ya mambo yanayoweza kupatikana katika ulimwengu halisi na yasiyowezekana huwa mdogo sana.

Tunakubaliana na maoni ya Wamitila (khj) na kufafanua miujiza kama matendo au matukio ambayo yanatendeka kiajabu bila matarajio yoyote ya kuwezekana kwayo; Matukio yanayotendeka katika ulimwengu mwingine wa kifantasia usio wa kawaida na huwa ajabu kwa watendewa mambo haya.

Maudhui ya miujiza yamejitokeza katika *Utenzi wa Nabii Isa* na yameendelezwa zaidi na matendo ya mhusika mkuu Nabii Isa ambayo ni matendo yanayoonyesha sifa za kiuhalisia ajabu.

Katika utenzi huu, makundi mawili yameonyesha misimamo miwili kinzani. Hata hivyo, ni dhahiri kuwa Nabii Isa alitenda miujiza. Kuhusu madai haya yetu, Nabii Isa alitenda miujiza kama vile kuwawezesha vipofu kuona; Nabii Isa aliwaponya watu wenye macho pofu na kuwafunulia macho yao (ubeti 422, 425). Miujiza hii ya Nabii Isa pia imejitokeza kwenye kitabu cha *Mathayo* 9:27-31 ambapo Biblia takatifu inaeleza kuwa Yesu alipoingia chumbani, alifuatwa na vipofu wawili waliomlilia na kumwomba kuwa, "Yesu mwana wa Nazarethi, tuonee huruma". Yesu alipowauliza kama walikuwa na imani kuwa angewaponya walionyesha imani yao kwa kuitikia. Yesu aliwagusa kwenye macho na wakaweza kuona (Mtazamo wa dini ya ukristo).

Kuhusu swala la uumbaji, Nabii Isa aliunda ndege kwa udongo aliofinyanga na ndege hao wakaweza kupaa waliporushwa. Baadhi ya sifa hizi ni za kiuhalisia ajabu na zilidhihirisha kuwa Nabi Isa alikuwa na uwezo zaidi kuliko binadamu wa kawaida (beti 452,472).

Jambo jingine la kimiujiza alilolifanya Nabii Isa ni kumtajia yule jamaa aliyeuliza chakula alichokila wakati wa asubuhi na chajio, maji aliyoyatumia, pesa za mfukoni na hata akiba ambayo huyo jamaa alikuwa nayo nyumbani. Huyo mtu alipodhibitisha ukweli wa mambo aliyotajiwa, alikosa kinywa cha kusema na baadaye akakubali kuwa kweli Isa ni Nabii (beti 380-382).

Kule kuzaliwa kwa Nabii Isa bila baba pia ni jambo la kiajabu kwani ni kinyume na hali halisi katika jamii; Nabii Isa alizaliwa bila mama kuonana kimwili na mume (ubeti 588) ila kwa mtume kumvivia tu Mariyamu nguo na akapata mimba ya mtoto Nabii Isa.

Kwa jumla, katika utenzi wetu tumeunga mkono maoni ya Fronz Roh kwa majibu wa Wamitila (2003) kuwa matendo ya kiuhalisia ajabu ni ya kifantisia na ya kiajabu, jambo hili limedhihirika katika utenzi huu.

**3.4 MALEZI NA NAFASI YA WANAWAKE**

Mdee nw (2011), malezi ni namna ya kumlea mtu au mtoto kwa mujibu wa taratibu zilizokubalika; makuzi, ulezi, lisha, uangalizi.

Kulingana na Tuki (2004), malezi ni njia ya ukuzaji wa mtoto kwa kutarajiwa kufuata tabia na mwenendo unaostahiki; makuzi, funzo.

Tunakubaliana na maoni haya na kufafanua zaidi kuwa malezi ni namna ya kipekee ya kumlea mtu au mtoto huku akitarajiwa kuwa atafuata tabia na mwenendo unaokubalika katika jamii. Basi kulingana na madai haya, asiyelelewa kwa namna ya kufuata taratibu zinazokubalika katika jamii husika atatazamwa kama kiruka njia kwani atakuwa na tabia zinazokiuka maadili katika jamii.

Dini ya uislamu inatilia mkazo umuhimu wa 'matunzo' ya watoto na inaonya vikali wazazi wasizembee. Qurani inataja kuwa:

*'Wala msijitie wenyewe katika maangamizi (2:145)'.*

Pia inasisitiza usawa wa jinsia zote (Jopo la maulamaa-misri 2005).

Maudhui ya malezi yametaliwa sana katika *Utenzi wa Nabii Isa*. Uzazi na malezi ni maswali mawili yanayohusiana na ndoa na malezi ya wana, mara nyingi katika jamii nyingi za kiafrika ni jukumu la wanawake kuwalea watoto.
Utenzi huu umeonyesha kuwa kuna wahusika waliojikita katika majukumu ya kusaka na vile vile kuwalea watoto.

Mkewe Imrani aliomba sana ili apate mimba na amzae mwana wa kiume. Mungu alipojibu maombi yake, alipewa mtoto lakini sasa akiwa ni wa kike (beti 51). Hata hivyo, kifo cha mamake Mariyamu kilimwacha Mariyamu akiwa na babake Bwana Imrani pekee. Jambo hili lilimfanya Bwana Imrani ajikaze vilivyo na kumlea mwanawe kwa mafunzo mazuri ya kidini (Ubeti 55).

Hata hivyo, malezi haya yanaendelezwa zaidi pale ambapo mwana anachukuliwa na Zakaria ambaye pamoja na mkewe walimlea Mariyamu kwa mafunzo mengi ya kidini (Ubeti 65).

Katika jamii hii ya uswahilini, malezi ni moja kati ya majukumu ya jamii, hii ndiyo sababu watu wengi wanang`ang`ana kuwa wapewe mwana (Mariyamu (ubeti 61).

Malezi haya ya Mariyamu yaliwahusisha aila ya Zakaria na jambo la ajabu ni kuwa hata Mola mwenyewe alileta vinono kila siku kwa Binti Mariyamu.

Tofauti na malezi ya Mariyamu, malezi ya Nabii Isa yalikuwa ni wajibu wa Mwanamke pekee (mama Mariyamu), tangu alipopata mimba hadi kuzaa kwake na hata baadaye. Jamii

ya Mariyamu haikushughulika na malezi ya Isa ila ilitupa lawama kwa Mariyamu ikimlaumu kwa kupata mtoto pasi na kuolewa (beti 282-297).

### 3.5 SHARIA ZA TORATI.

Sharia ni kanuni za kidini pamoja na imani katika dini ambazo ndizo huongoza jamii katika ujumla wake.

Torati kwa upande mwingine ni fundisho, mwongozo au sharia. Katika uislamu, torati inataja vitabu vitano vya kwanza vya Tanakh. Torah basi ni msingi muhimu wa kidini ya kiyahudi ya maadili yanayotegemea utekelezaji wa maagizo (Mitzvot 613).

Katika *Utenzi wa Nabii Isa,* Mola alimpa Musa sheria za torati ili awape waisraeli wafuate katika imani yao katika dini.

Mtume Musa basi aliweka msingi mzuri wa uongozi madhubutu kwa waisraeli kwani ndiye aliyewaongoza kabla ya Nabii Isa na ndiye aliyewatendea wana Israeli miujiza kabla ya miujiza aliyoitenda Nabii Isa.

Kuja kwa Nabii Isa basi kumeendeleza tu msimamo aliokuwa nao mtume Musa kwa kuendeleza sharia za taurati.

Jambo hili la mahubiri na sheria za taurati katika asasi ya kidini pia limezungumziwa katika Bibilia takatifu. Katika kitabu cha *Kutoka* 20:1-17 na K*umbukumbu la torati* 5:1-21

Na Mungu alisema maneno haya:

*"Mimi ndimi Mola wako aliyewatoa Israeli kutoka kwenye nchi ya utumwa, msiwe na miungu wowote ila Mimi, msijiundie masanamu kwa sura yoyote iliyo mbinguni au duniani, msitumie jina la Mola vibaya kwani Mola hatakosa kumwonea makosa anayetumia jina lake vibaya, kumbuka kutii siku ya sabato, heshimu baba na mama yako ili uishi maisha marefu duniani, usiue, usijihushishe na ukahaba, usiibe, usitoe ushuda usio wa kweli dhidi ya jamii yako, usitamani nyumba, Bibiye, kijakazi wala dume wake jirani"* (*Kutoka* 20:1-17) Mtazamo wa dini ya kikristo).

**3.6 NDOA**

Ndoa ni makubaliano rasmi baina ya mwanamume na mwanamke kuwa waishi pamoja kama mke na mume. Kulingana na Bibilia takatifu, inadaiwa kuwa ndoa ya kwanza ilikuwa ya Adamu na Hawa katika shamba la Edeni pale ambapo waliishi na baadaye kuasi matakwa ya Mola, jambo lililowalaani na wakafukuzwa kwenye shamba la Edeni (*Mwanzo* 20:24-25). Hii inaonyesha kuwa ndoa ni asasi iliyoasiliwa na Mola mwenyewe.

Asasi ya ndoa ndiyo inayoendeleza ukuaji wa jamii na ndiyo msingi wa familia kwani kutokana na ndoa watoto wanazaliwa na kuendeleza ukuaji wa jamii.

Maudhui ya ndoa yameshamiri katika utenzi wa Nabii Isa. Huu ni utenzi wenye msingi wake katika uislamu unaohimiza sura ya ndoa. Hivyo basi maudhui ya ndoa katika utenzi huu yameendelezwa hasa kwa asasi ya dini. Katika utenzi huu, ndoa kati ya Bwana Imrani na mkewe iliendelezwa kwa imani kuu katika dini ya kiislamu. Bwana Imrani na mkewe waliishi kwa imani katika dini hata walishinda msikitini wakiabudu kwa kuwa alikuwa

imamu wa dini (beti 21-22) pamoja na mkewe walisimamia ibada msikitini kuabudu manani (ubeti 22).

Kuhusu asasi hii ya ndoa, mtume Zakaria pia aliishi na mkewe na walimlea Mariyamu kwa mafunzo mema ya kidini. Kuzaliwa kwa Nabii Isa katika familia ya Mariyamu hata hivyo ni tofauti na maendeleo ya kindoa kwani Nabii Isa alizaliwa kimiujiza baada ya mtume wa Mungu kumvivia nguo Mariyamu na baadaye akapata mimba ya mwana Nabii Isa kishaye kumzaa na kumlea kwa mafunzo ya kidini.

## 3.7 MAADILI

Asasi ya dini imejitokeza kuwa kuu dhidi ya maudhui mengine kwani ndiyo huendeleza maudhui mengine.

Mtunzi wa *Utenzi wa Nabii Isa* amewasawiri wahusika wake kama waadilifu na uadilifu huu hasa umeendelezwa zaidi na asasi ya dini.

Katika utenzi huu, Maadili yameonyeshwa kuwa msingi wa maisha ya binadamu kwani ndiyo huongoza matendo yote ya binadamu hasa katika malezi.

Imrani na mkewe walionyesha uadilifu wa hali ya juu katika matendo yao kama vile kukubali kumlea Mariyamu, hasa katika msingi wa dini, mtume Zakaria alionyesha uadilifu katika maisha yake ya malezi na kumlea Mariyamu na Mariyamu mwenyewe pia akawa mwadilifu vile vile kwani alilelewa katika sheria na kanuni za dini (ubeti 87).

Mariyamu aliendeleza uadilifu alioupokea kutoka kwa wazazi wake Bwana Imrani na mamake na vilevile kutoka kwa familia ya Mtume Zakaria aliyekuwa mlezi wake.

Nabii Isa pia alionyesha uadilifu kwa njia nyingi kama: Kuendeleza dini kwa kuhubiri mahakamani na misikitini pia na kuendeleza yote aliyoagizwa na Mola.

## 3.8 USALITI NA DHULUMA

Mdee nw (2011), wanaeleza kuwa Usaliti ni utoaji habari za siri za nchi au mtu kwa adui wake; tendo la kumdanganya mpenzi kwamba unampenda na kumwacha peke yake.

Pia wamefafanua dhuluma kama kitendo cha kumnyima mtu haki au stahiki yake; uonevu. Kulingana na Tuki (2004), dhuluma ni kufanyia mtu kitendo kisicho cha haki; onea, nyanyasa au hata kunyanganya mtu pesa au mali.

Katika *Utenzi wa Nabii Isa*, maudhui ya usaliti yamejitokeza pale ambapo Nabii Isa pamoja na wanafunzi wake waliishi, kula na kunywa pamoja lakini baadaye mmoja miongoni mwa wafuasi wake ndiye aliyemchochea kwa kumtaja kwa wahalifu waliotarajia kumwua (beti 785-790). Nabii Isa alipangiwa njama ya kuwawa, jambo ambalo Mola alibadilisha kwa kuleta mtu ambaye alimfananisha na Nabii Isa kisura na baadaye mtu huyu akateswa, akawawa, akasulubiwa msalabani na wahalifu wale wakidai kuwa huyu alikuwa ni Nabii Isa mwenyewe.

Madai ya wahakiki wengi kama Wa Mberia (1989) na Achieng (2012) kuwa majagina wanakumbwa na masaibu mengi na vilevile wana maadui wengi ni ya kweli kwani Nabii Isa katika *Utenzi wa Nabii Isa* alikumbwa na matatizo mengi, sio kutofautiana kuhusu unabii wake kwa wana wa Israeli, waisraeli walihitilafiana kuhusu iwapo Isa ni Nabii au sio (beti

528-630), sio njaa akiwa pamoja na wanafunzi wake, sio kusalitiwa kwake kwa mmoja wa wanafunzi wake (beti 785-790).

### 3.9 KIFO NA UFUFUKAJI.

Kifo kimeangaziwa katika Biblia kuwa chanzo chake ni dhambi waliyotenda wanadamu wa kwanza katika shamba la Edeni (*Mwanzo* 3:19)

> *"Huwabidi mfanye kazi kwa bidii na kutoa jasho ili kuwezesha udongo kutoa rutuba hadi mtakaporudi mchangani mlikoumbwa. Kwani mliumbwa kutokana na udongo na mtakuwa udongo tena"*

Kwa mujibu wa Biblia takatifu, Kuhusu ufufukaji, Nabii Isa aliwafufua maiti. Kuna vifungu vingi katika Biblia vinavyoeleza swala hili la ufufukaji; katika kitabu cha *Mariko* 5:35-43, Yesu alimfufua binti wa mkuu wa sinagogi (Jairo), *Luka* 7:11-16 ndipo Yesu asemekana kufufua maiti kule Naini na maiti huyu akiwa ni mwana wa mjane, mwanawe wa pekee.

Matukio mengine yanayodhihirisha ufufukaji katika Biblia ni pamoja na Yesu mwenyewe kusema kama dhibitisho kuwa ana uwezo wa kifo na ufufukaji (*Yohana* 11:25-27).

> *" ..mimi ndimi huo ufufuo na uzima, yeye aniaminiye mimi ajapokufa*
> *atakuwa anaishi, naye kila aishiye na kuniamini hatakufa kabisa*
> *hata milele."*

Kifo kwa mujibu wa Mzenga (1977) kimesawiriwa kwa njia tofauti kwani walioaga waliweza kufufuliwa na Nabii Isa (beti 507-518).

Katika utenzi huu vilevile, kifo kimesawiriwa kuwa hakimhusu Nabii Isa mwenyewe kama kilivyo katika Biblia takatifu kwani baada ya Nabii Isa kusalitiwa, Mungu alimleta mja katika

sura yake Nabii Isa, akadhulumiwa na kusulubiwa badala ya Nabii Isa mwenyewe (beti 794-802) tofauti na maelezo ya Biblia katika dini ya ukristo kuwa Nabii Isa mwenyewe alisalitiwa, akadhulumiwa na kusulubiwa hadi akafa na baadaye kufufuka baada ya siku tatu (*Luka mtakatifu* 24:1-10, *Yohana* 20:1-23, *Mathayo* 28:1-20).

## 3.10 HITIMISHO.

Katika sura hii tumeweza kuhakiki *Utenzi wa Nabii Isa* kimaudhui kwa kujikita katika misingi ya nadharia ya Uyakinifu wa Kijamii. Kwa kupitia nadharia hii, tumedhibitisha kuwa maudhui ya ushujaa, dini, miujiza, malezi na nafasi ya wanawake, sharia za torati, ndoa, maadili, usaliti na dhuluma pamoja na kifo na ufufukaji yamejitokeza bayana katika utunzi wake Musa Mzenga (1977), *Utenzi wa Nabii Isa.*

Maudhui haya yamebainika wazi katika jamii hii ya utunzi na baadhi ya wahusika wameathirika kwa namna tofauti walipoingiana katika harakati za kukidhi mahitaji yao kiuchumi na kijamii.

Baadhi yao wamefanikiwa pakubwa na wengine wakaangamia kwa sababu ya hiana na vitimbi vyao ambavyo havikuwa na mwisho mwema. Ili tuweze kufafanua vizuri vile mafanikio na maangamizi haya yalivyoshamiri, imetupasa tushughulikie jinsi maudhui haya yameibua athari mbalimbali katika sura ya nne inayofuata.

# SURA YA NNE.

## ATHARI ZINAZOIBULIWA NA MAUDHUI HAYA PAMOJA NA UYAKINIFU WA MAUDHUI HAYA KATIKA JAMII YA JADI NA KISASA.

### 4.0 UTANGULIZI.

Katika sura hii tumeangazia jinsi maudhui yanavyoibua athari mbalimbali, zikiwa ni athari chanya na hasi. Tumerejelea *Utenzi wa Nabii Isa* katika kufafanua athari hizo na kuonyesha uyakinifu na uamilifu wa maudhui hayo katika jamii.

Kwa mujibu wa Lucaks (1962), uyakinifu wa kijamii una uwezo wa kusawiri jamii katika ukamilifu wake na kuonyesha hatua zake za kimabadiliko, ukamilifu huu kwa mujibu wa Lucaks (1962) hupatikana binadamu anapotimiza mahitaji ya kimsingi maishani kama: lishe, uzazi, faraja za kimwili, burudani, utangamano, usalama na maendeleo. Endapo mahitaji haya hayajakidhiwa, ni lazima binadamu apambane na hali zinazokwaza ili ajikomboe na aweze kuridhika na hali anuai za maisha. Hii ndio sababu kuu ya binadamu kung'ang'ana maishani na kujaribu kutimiza mahitaji haya saba ya kimsingi katika maisha ya binadamu (Malonowski kwa mujibu wa Gatakaa 2012).

Uchunguzi wetu wa kimaudhui katika *Utenzi wa Nabii Isa* huonyesha kuwa maudhui mbalimbali yameshamiri. Matendo ya wanajamii yamechangia kujengeka kwa maudhui haya ambayo yameibua athari zake kwa jamii ya wakati huo na sasa.

Katika sura hii hatuna budi basi kuangazia athari chanya na hasi zinazoibuliwa na maudhui haya ya ushujaa, ndoa, dini, sharia za torati, maadili, dhuluma na usaliti, maadili, kifo na ufufukaji na malezi na nafasi ya wanawake.

**4.1 USHUJAA.**

Kulingana na maelezo yetu katika sura ya tatu, jagina huzaliwa ili kutimiza mahitaji ya jamii katika kipindi mahususi na matatizo ya jamii huwa yanaibuliwa na maswala ya kisiasa, kiuchumi na kijamii na hayawezi kujiondoa hadi kuibuka kwa jagina atakayeyatatua matatizo hayo. Majagina basi huzuka ili kutosheleza mahitaji ya kishujaa yanayohitaji masuluhisho.

Ushujaa kwa mujibu wa Malinowski anavyonukuliwa na Gatakaa (2012) ni muhimu katika ukombozi dhidi ya hali dhalilishi za kuzorotesha aidha kiuchumi, kisiasa na kijamii.
Mashujaa wa kidini wana sifa zinazowatambua kama majagina wa kidini na mfano ni kama vile Musa.

Katika *Utenzi wa Nabii Isa*, kuzuka kwa Musa hapa kama shujaa wa kidini kuliwapa waisraeli mwangaza kuhusu sharia za kidini na kuwaongoza kwa kuwapa mwelekeo wa maisha mapya ambayo yalihusiana na imani katika dini hata ingawa wengine waliasi mafunzo ya Musa na kujikita katika matendo duni ya kuabudu masanamu kama walivyofanya awali kabla ya Musa.

*Utenzi wa Nabii Isa* umewasawiri Musa na Nabii Isa kama mashujaa wa kidini ambao walikuwa na majukumu ya kuzindua jamii dhidi ya dhambi. uzinduzi wao kwa jamii ulikuwa na athari chanya kwa jamii hiyo kwani baadhi ya wana wa Israeli waliweza kufahamu umuhimu wa dini na kuweza kuwa na imani katika dini ya uislamu.

Miujiza aliyoitenda Nabii Isa iliwaokoa watu wa Israeli dhidi ya maafa kwani aliwafufua maiti (beti 511-512).

Hata ingawa matendo ya Musa na Nabii Isa ya kishujaa yaliwafaidi wanajamii, waliweza kujipata matatani vilevile japo walikuwa mitume wa Mola. Mwanzo, mtume Musa na Nabii Isa waliweza kupata maadui wengi, hasa wale ambao hawakumtazama Nabii Isa kama Nabii na kuhitilafiana na wenzao waliokuwa wafuasi wa Nabii Isa. Hii inaonyesha kuwa majagina wanakumbwa na matatizo mengi katika mazingira yao wanapojaribu kukomboa jamii zao kutokana na hali dhalilishi za kurudisha nyuma maendeleo. Haya yameoana na maoni yake Wa mberia (1989) kuwa majagina hukumbwa na masaibu mengi. Hata hivyo, kuzuka kwa mashujaa hawa wawili kulileta vitambulisho wa kijamii miongoni mwa wanajamii wa Israeli kwani walitoa sheria za kidini zilizoigwa na watu.

**4.2 DINI.**

Dini ni asasi muhimu sana katika maisha ya binadamu kwa kuwa inahusishwa na binadamu kwa njia ya moja kwa moja.

Gatakaa (2012) aeleza kuwa imani na nguvu zote za binadamu hutiwa kwenye dini na hasa kiumbe mwenye nguvu anayetegemewa na wafuasi wa dini hiyo. Maoni haya ya Gatakaa (2012) yanafafanua sababu ya kuwa si rahisi kutenganisha dini na maisha ya binadamu.

Mtunzi Mzenga (1977) amesawiri baadhi ya wahusika wake kuwa wametegemea nguvu hizi za juu kama suluhisho la matatizo yao. Kwa mfano, Bwana Imrani na mkewe walipohitaji mwana, waliomba mola ili awape mwana wa kiume na Mungu akajibu maombi yao kwa kuwapa mwana wa kike (Mariamu). Bwana Imrani basi amesuluhisha matatizo ya kupata mwana kwa sala ya kidini.

Isa na wanafunzi wake waliomba jangani ili wapate chakula na mwishowe walipewa kutokana na maombi aliyofanya Nabii Isa. Chakula chenyewe kikiwa kinaitwa maida. Kilikuwa kitamu kisichomithilika (beti 746-761).

Matendo mengi ya Nabii Isa ya kimiujiza yenye uhalisia wa kiajabu kama vile kuwezesha wafu kufufuka (beti 511-512), kuwezesha vipofu kuona (beti 422-425), kuunda ndege walioweza kupaa waliporushwa (beti 452,472), kumtajia yule jamaa aliyemwuliza kuhusu chakula alichokila wakati wa asubuhi na chajio, maji aliyoyatumia, fedha za mfukoni na akiba ambayo huyo jamaa alikuwa nayo nyumbani yametegemea imani yake na ya wafuasi wake katika dini ya uislamu.

Ni dhahiri kulingana na mtunzi huyu kuwa binadamu hutegemea dini sana hasa dini ya uislamu katika maisha ya kila siku na hasa katika kupata suluhisho dhidi ya matatizo anayokumbana nayo maishani.

Tunaunga mkono na kuamini kuwa dini ina sifa bora za kufuatwa na binadamu na ni nguzo ya uadilifu, yenye kufunza desturi nzuri na kumpa mtu utulivu wa moyoni.

Imani katika dini imefanya watu kuishi kwa amani duniani tangu jadi na kwa imani kuwa baada ya maisha ya ulimwengu kufikia kikomo kuna maisha mengine ambapo kila mja atapata thawabu kwa kutegemea alivyoishi.

Mashujaa wa kidini hapa wametimiza jukumu la kukuza tamaduni za kidini miongoni mwa wanajamii kwa kuhimiza uadilifu na kufunza desturi nzuri. Jambo hili limeoana na maoni ya Achieng (2012) kuhusu majukumu ya mashujaa katika jamii zao kama kukuza tamaduni za jamii hiyo.

## 4.3 MIUJIZA.

Matendo ya kiuhalisia ajabu ya Nabii Isa na mtume Musa ndiyo yanayochangia zaidi katika kuendeleza maudhui ya miujiza. Haya matendo huwafanya kuwa majagina wa kidini kwani Nabii Isa ameweza kujitokeza kuwa na sifa nyingi zinazomtambua kama jagina kama vile zile sifa anazoeleza Wa mutiso (1985), Wa mberia (1989) na Achieng (2012). Miujiza hii ndiyo iliyoendeleza matumaini ya jamii na imani yao kuhusu dini.

Katika jamii, sifa hizi za majagina zinawapa majukumu mengi yanayokamilisha mahitaji ya jamii kama anavyodokeza Casey (2004) katika mswada wake *Unlikely Heroes and their roles in Fanfasy Literature.* Casey anaeleza kuwa majagina wana majukumu yanayofaidi jamii wala sio kujinufaisha wenyewe. Matendo yao yanawapa nafasi ya kuwa watetezi wa wanajamii wa tabaka la chini na kuwapa mwelekeo wa kujifaidi.

Majagina pia wanapigana na hali zote kinzani za kuleta utata. Mara nyingi mzuri anaibuka kuwa mshindi. Kwa mfano, katika *utenzi wa Nabii Isa*, mhusika mkuu Nabii Isa anashinda shauku kuwa yeye si Nabii (ubeti 614-615). Wakati Nabii Isa alipata pigo la usaliti, Mungu aliweza kuumba mtu kwa mfano wake Nabii Isa aliyepatwa na dhuluma na mwishowe kuwuawa badala ya Nabii Isa.

Mwandishi Casey (2004) pia anadai kuwa kama majagina wengine wa kitamaduni, majagina wote wanawahudumia wafuasi wao.

Tunaafikiana na maoni yake Casey (khj) na kusema kuwa mtunzi Mzenga (1977) alionyesha haya kwa kumsawiri Nabii Isa kama mhusika mwenye huruma aliyeombea wanafunzi wake

na wakapewa chakula (beti 746-761), alifufua maiti, alipoza vipofu (beti 422, 425) na yote kwa lengo la kuokoa watu katika jamii na kuwaonyesha mapenzi.

## 4.4 MALEZI NA NAFASI YA WANAWAKE.

Malezi yanayojitokeza katika jamii nyingi yanaongozwa na wanawake. Hata hivyo, Katika *Utenzi wa Nabii Isa,* maudhui ya malezi yametaliwa sana na huhusiana pakubwa na ndoa pamoja na uzazi.

Mwanzo, uzazi unaojitokeza katika utenzi huu ni wa aina yake kwani kuna uzazi unaotokana na ndoa halali kati ya mke na mume na kwa upande mwingine kuna uzazi wa kimiujiza uliofanyika kwa Mariyamu wakati alipopata mimba ya Nabii Isa kwa uwezo tu wa Mola bila kukutana kimwili na mume kama tulivyoeleza katika sura ya tatu. Haya yanatoa mafunzo makuu kwa jamii ya wakati huo na sasa kuwa Mola ana uwezo wa kupanga mambo yake ya uzazi kwa njia nyingi na matendo yake hayana pingamizi hata yakiwa ya kiajabuajabu, athari basi ikawa ni chanya kwa jamii zote za jadi na sasa kwa kuwapa imani kuu katika dini.

Mke wa Imrani aliomba sana apate mimba na baadaye akapata mwana wa kike (ubeti wa 51 (kwa bahati mbaya mamake Mariyamu afa na kumwacha na baba (ubeti 55), Bwana Imrani ambaye anabaki kujikaza kisabuni kumlea mwanawe.

Hata hivyo, mwana anachukuliwa na Zakaria ambaye wanamlea pamoja na mkewe, mama mdogo wa Mariyamu (ubeti 65). Haya yamekuwa na athari ya kuzindua jamii za jadi na leo kuwa malezi ni majukumu ya jamii nzima wala sio mzigo tu kwa mtu mmoja ambaye mara nyingi hutazamwa kuwa ndiye mama mzazi kama inavyojitokeza katika malezi ya Nabii Isa yaliyofanywa na mamake Mariyamu pekee na hali hii ilimtupia Mariyamu lawama kuwa alileta aibu katika jamii kwa kupata mwana bila kuolewa (beti 282-297).

## 4.5 SHARIA ZA TORATI.

Sharia na kanuni za kidini pamoja na imani kubwa katika asasi ya dini ya uislamu na hata dini zingine zimekuwa mhimili mkuu katika kuongoza azazi zingine katika jamii nyingi. Sharia hizi zinatumika kuongoza jamii nyingi katika kiwango cha familia, taifa na hata kimataifa.

Katika jamii rejelewa katika *Utenzi wa Nabii Isa*, sharia za torati ndizo ziliongoza maadili ya watu na zilisisitiza sana katika imani ya dini ya uislamu. Mwanzo, mtume Musa alionyesha umuhimu wa kufuata sheria hizi na baadaye Nabii Isa akaongoza kwa kutoa msisitizo zaidi.

Sharia hizi pia hutumika kuwaongoza waumini katika ukristo kama zinavyojitokeza katika kitabu cha *Warumi* 13:8-10.

> *"Msiwiwe na mtu chochote, isipokuwa kupendana; kwa maana ampendaye mwenzake ametimiza sheria. Maana kule kusema usizini, usiue, usiibe, usitamani; naikiwapo amri nyingine yoyote, inajumlishwa katika neno hili, ya kwamba, Mpende jirani yako kama nafsi yako. Pendo halimfanyii jirani neno baya; basi pendo ndilo utimilifu wa sheria."*

Kwa jumla, sharia za kidini zina jukumu la kukuza na kuendeleza tamaduni za dini hiyo.

## 4.6 NDOA.

Ndoa ni asasi ya kimsingi katika uendelezaji wa jamii kwa jumla. Asasi hii inahakikisha kukua na kuendelea kwa jamii na ndiyo msingi wa familia.

Gatakaa (2012) anamuunga mkono Robert anaposema kuwa ndoa inapaswa ijengwe katika misingi ya mapenzi, vinginevyo haiwi kwa sababu haitadumu.

Tunawaunga mkono wataalamu hawa katika madai yao na kusema kuwa ni kweli kwani ndoa inajengwa kwa misingi ya maelewano makubwa na mapenzi ya dhati. Kwa mujibu wa Mzenga (1977), mwandishi huyu ametusawiria ndoa kati ya Bwana Imrani na mkewe walioomba Mola awape mwana wa kiume kama zawadi yao katika ndoa. Bwana Zakaria pia aliishi na mkewe pamoja na mwana Mariyamu lakini yote haya yalidumu tu kwa sababu ya mapenzi waliyokuwa nayo. Jamii hii basi inafaidi kutokana na uendelezaji wa jamii kwa misingi ya ndoa, lakini, mwandishi yuyu huyu pia anatusawiria hali ya uendelezaji wa jamii kiuzazi pasipo na ndoa; yaani, mtoto kuzaliwa kimiujiza bila baba kama ilivyo hali ya uzazi wa Nabii Isa bin Mariyamu.

Jamii hii basi ni ya kipekee ambapo ndoa sio njia pekee ya kuendeleza uzazi bali Mola amesawiriwa kuwa na uwezo mkubwa zaidi wa kutenda yasiyowezekana kikawaida na hii ni muhimu katika uelewa wa jamii.

## 4.7 MAADILI.

Tunaafikiana na ufafanuzi wa Mdee *nw* (2011), kama tulivyoeleza hapo awali katika sura ya tatu kuwa maadili ni mwenendo au tabia njema inayokubalika katika jamii au katika kazi.

Asasi ya dini imejitokeza kama mhimili mkuu wa kuendeleza maadili katika jamii yoyote ile.

Katika jamii rejelewa katika *Utenzi wa Nabii Isa*, uadilifu wa baadhi ya wahusika kama vile Bwana Imrani na mkewe pamoja na mtume Zakaria na mkewe umewezesha kukuwa kwa binadamu katika misingi mizuri ya kidini chini ya sheria za kidini kama vile malezi mazuri aliyofanyiwa Mariamu kwao na hata kwa Zakaria. Hii inaondoa maovu katika jamii na hii ndiyo sababu wazazi wa Mariyamu walisifika sana katika jamii yao kwa heshima yao (beti 244,249) Pia kwa sababu ya maadili, Mariyamu anachelea kufikiria vibaya kuwa yeye ni mwovu (ubeti 121).

Katika utenzi huu, Maadili ya jamii yanalindwa na kila mwanajamii na hawachelei kuuliza pale panapotokea hila katika jambo; kwa mfano, wanajamii wanamkazia Mariyamu macho na kumtaka aeleze ni kwa nini amepata mimba haramu, Nabii Isa anakanya watu dhidi ya maovu kama vile kuwa haramu (ubeti 664). Aidha, anasusia wizi na dhuluma (beti 330-331). Nabii Isa pia alimkataza mtu ana kwa ana kuhusu wizi (ubeti 333) na haya yote yanachangiwa na uadilifu wake.

**4.8 DHULUMA NA USALITI.**

Ufafanuzi wetu wa usaliti kama utoaji wa habari za siri za nchi au mtu kwa adui wake kama tulivyoeleza katika sura ya tatu unathibitishwa katika *Utenzi wa Nabii Isa* ambao una ukuruba mkubwa sana na tenzi zingine za kidini. Katika *Utenzi wa Nabii Isa*, usaliti umejitokeza pale ambapo majambazi na wakuu wa Roma walipomlaghai mfuasi mmoja wa Nabii Isa kwa kumwahidi tuzo la kupewa uwaziri, kila kitu kizuri na nyumba ya fahari pamoja na mali ya kutumia (ubeti 785). Hapo ndipo mwanafunzi wake huyo mmoja alipomsaliti kwa kuwapeleka askari hadi mafichoni mwa Nabii Isa na wanafunzi wengine (beti 787-790).

Usaliti wa aina hii pia umejitokeza katika kitabu cha *Luka mtakatifu* 22:3-6 na 22:21-23 Bibliani pale ambapo katika kifungu cha kwanza tunapata maelezo kuwa shetani alimwingia Yuda Iskarioti aliyekuwa mmoja wa wafuasi thenashara wa Yesu kristo na akasema na wakuu wa makuhani na majemedari jinsi atakavyoweza kumtia mkononi mwao, wakuu wakafurahi na kupatana naye na kumpa pesa baadaye. Yuda akakubali na kutafuta nafasi ya kumsaliti. Vilevile katika kifungu cha pili mtawalia (khj), Yesu Kristo anasema baada ya kutambua kuwa atakayemsaliti ni mmoja wa wafuasi,

> *"Walakini, tazama, mkono wake yeye anayenisaliti upo*
> *hapa pamoja name mezani, kwa kuwa mwana wa Adamu*
> *aenda zake kama ilivyo kusudiwa; lakini, ole wake mtu*
> *yule amsalitiye! Wakaanza kuulizana wao kwa wao, ni*
> *yupi miongoni mwao atakayelitenda jambo hilo."*
> (Mtazamo wa kikristo)

Usaliti huu ndio uliochangia dhuluma iliyotokea katika jamii hii. Hata hivyo, katika *Utenzi wa Nabii Isa,* maudhui ya dhuluma yamejitokeza kwa njia ya kipekee kwani wale makuhani walidhani walimdhulumu Nabii Isa kumbe kiajabu tu Mola alileta mtu aliyechukua sura ya Nabii Isa na huyu ndiye aliyetekeleza mahitaji ya dhuluma katika utenzi huu kwani makuhani walimtesa wakidhani alikuwa Nabii Isa mwenyewe na hatimaye kumwua (beti 794-802).

Kulingana na mwandishi wa makala ya kidini, Ellen (2001), *The Desire of Ages*, Msaliti wa Yesu Kristo Yuda Iskarioti alidai kuwa iwapo Yesu atasulubishwa, masaibu hayo yangepita na kusalitiwa kwake hakungeleta mabadiliko yoyote kuhusu kifo chake kwani kufa kwake kulitabiriwa (Mtazamo wa kikristo).

Katika jamii hii basi, athari za usaliti na dhuluma ni kuwa mtazamo wa jamii umeweza kupanuka na kumtazama Mungu kama muweza kutokana na uwezo wake wa kumleta mtu katika sura ya Nabii Isa ili kudhulumiwa na kusulubishwa hadi kifo chake badala ya Nabii Isa mwenyewe. Mungu basi alifahamu kuwa Nabii Isa hakufa bali aliwapumbaza wahalifu hao.

## 4.9 KIFO NA UFUFUKAJI.

Kifo kimeangaziwa katika Biblia kuwa chanzo chake ni dhambi waliyotenda wanadamu wa kwanza katika shamba la Edeni (Mwanzo 3:19)

> *"Huwabidi mfanye kazi kwa bidii na kutoa jasho ili kuwezesha*
> *udongo kutoa rutuba hadi mtakaporudi mchangani mlikoumbwa.*
> *Kwani mliumbwa kutokana na udongo na mtakuwa udongo tena".*

Kwa mujibu wa Biblia takatifu, kuhusu ufufukaji, Nabii Isa aliwafufua maiti. Kuna vifungu vingi katika Biblia vinavyoeleza swala hili la ufufukaji; katika kitabu cha *Mariko* 5:35-43, Yesu alimfufua binti wa mkuu wa sinagogi (Jairo), *Luka* 7:11-16 ndipo Yesu asemekana kufufua maiti kule Naini na maiti huyu akiwa ni mwana wa mjane, mwanawe wa pekee.

Matukio mengine yanayodhihirisha ufufukaji katika Biblia ni pamoja na Yesu mwenyewe kusema kama dhibitisho kuwa ana uwezo wa kifo na ufufukaji (*Yohana* 11:25-27).

> *" ..mimi ndimi huo ufufuo na uzima, yeye aniaminiye mimi*
> *ajapokufa atakuwa anaishi, naye kila aishiye na kuniamini*
> *hatakufa kabisa hata milele."*

Kifo kwa mujibu wa Mzenga (1977) kimesawiriwa kwa njia tofauti kwani walioaga waliweza kufufuliwa na Nabii Isa (beti 507-518).

Katika utenzi huu vilevile, kifo kimesawiriwa kuwa hakimhusu Nabii Isa mwenyewe kama kilivyo katika Biblia takatifu kwani baada ya Nabii Isa kusalitiwa, Mungu alimleta mja katika sura yake Nabii Isa, akadhulumiwa na kusulubiwa badala ya Nabii Isa mwenyewe (beti 794-802) tofauti na maelezo ya Biblia katika dini ya ukristo kuwa Nabii Isa mwenyewe alisalitiwa, akadhulumiwa na kusulubiwa hadi akafa na baadaye kufufuka baada ya siku tatu (*Luka mtakatifu* 24:1-10, John 20:1-23, *Mathayo* 28:1-20).

Hali hii inaonyesha kuwa Mungu ana uwezo dhidi ya kifo na hii ndiyo sababu alileta mja katika sura ya Nabii Isa aliyekabili dhuluma.

## 4.10 HITIMISHO.

Sura hii imechunguza athari mbalimbali zinzoibuliwa na maudhui yanayojitokeza katika *Utenzi wa Nabii Isa*. Hii ni kwa sababu utenzi huu umeangaziwa kwa uyakinifu wa kijamii, tumeweza kudhihirisha hali faafu ili utenzi huu uwe na uamilifu kwa jamii ya wakati huo na sasa huku tukitoa mifano  tunayodhania ni mwafaka.

Tumegundua kuwa athari hizi zimeboresha na zingine hasi zilizobomoa hali ya wanajamii kisaikolojia na kijamii.

## SURA YA TANO.

## HITIMISHO.

### 5.0 UTANGULIZI.

Hii ni sura ya mwisho inayohusu hitimisho la utafiti wetu.

Matokeo haya ndiyo yametuwezesha kupima nadharia tete zetu pamoja na malengo yetu ya utafiti. Hatimaye, katika sura hii tumetoa mapendekezo ya utafiti zaidi wa kimaudhui katika *Utenzi wa Nabii Isa*.

### 5.1 MUHTASARI WA UTAFITI.

Utafiti huu wetu uliazimia kuchanganua maudhui teule kama yanavyojitokeza katika *Utenzi wa Nabii Isa*. Tumeigawa tasnifu hii katika sura tano na kila sura imeumdwa kwa sehemu zake mbalimbali.

Katika sura ya kwanza, tumetalii utangulizi wa utafiti na hapa ndipo tumeeleza maswala ya kiutangulizi na ya kimsingi ya utafiti wetu huu. Maswala hayo ni pamoja na; mada ya utafiti, tatizo la utafiti, madhumuni ya utafiti, sababu ya kuchagua mada, nadharia tete, upeo na mipaka, msingi wa kinadharia, yaliyoandikwa kuhusu mada na njia za utafiti.

Katika sura ya pili, tumefafanua dhana ya maudhui pamoja na mihimili inayojenga na kuendeleza mbele maudhui na jinsi maingiliano yake yamejenga maudhui katika *Utenzi wa Nabii Isa.*

Sura yetu ya tatu imehusu uchanganuzi wa maudhui teule katika *Utenzi wa Nabii Isa* na sura ya nne imeangazia jinsi maudhui husika yameibua athari mbalimbali ambazo ni chanya na hasi kwa kurejelea *Utenzi wa Nabii Isa* na pia uyakinifu wayo katika jamii.

Sura ya tano ni ya hitimisho. Katika sura hii tumetoa muhtasari na maoni kuhusu tasnifu hii pamoja na mapendekezo ya kufanywa kwa utafiti wa kimaudhui zaidi katika *Utenzi wa Nabii Isa*.

Utafiti wetu umetuelekeza kutambua kuwa *Utenzi wa Nabii Isa* una maudhui ambayo yana uyakinifu katika jamii. Mtunzi Musa Mzenga, almaarufu, Ustadh Shirazi amefaulu kuyajenga na kuyaendeleza maudhui hayo teule katika kazi nzima kwa kupitia baadhi ya mihimili ambayo tumejadili kwa kifupi. Mihimili hii ndiyo inayositiri maudhui na pia ni nguzo muhimu ambazo kwazo maudhui hujengeka na kuendelezwa katika kazi yoyote ya kifasihi.

Katika kazi hii, mtunzi amethibitisha kuwa binadamu anastahili kuwa shujaa ili kufanikiwa kujinasua dhidi ya hali zote dhalilishi za kiuchumi, kisiasa na kijamii zinazomnyima utu wake. Pia ameonyesha kuwa dini ni asasi muhimu zaidi inayoendeleza asasi zingine katika maisha ya binadamu na Mola ana nafasi muhimu zaidi katika asasi ya dini kwani huamua na huamuru matukio yote katika mtalaa wa dini.

Pia amefaulu kuonyesha kuwa dini ni muhimu sana katika maisha ya binadamu. Amedhihirisha kuwa dini ina mafunzo bora kwa binadamu na baadhi ya mafunzo hayo ni; dini ni nguzo muhimu ya uadilifu yenye kufunza binadamu desturi nzuri, inampa mhusika utulivu wa moyo na pia kutoa suluhisho dhidi ya matatizo yanayokiuka uwezo wa binadamu.

Hali kadhalika, maudhui haya mbalimbali yameibua athari kadha katika maisha ya binadamu kwa kurejelea *Utenzi wa Nabii Isa* na pia jamii halisi. Kwa upande mmoja, yameboresha mwanadamu na kwa upande mwingine, yamebomoa. Kwa kuchunguza wakati wa utunzi na uandishi wa utenzi huu, tumetambua kuwa maudhui yaliyojengwa yalikuwa na uamilifu katika jamii ya wakati huo na sasa, hivyo basi uamilifu huo haujapitwa na wakati.

## 5.2 KUHUSU MALENGO YA UTAFITI.

Madhumuni yetu ya utafiti yametuongoza kubainisha yafuatayo:

Mtunzi Musa Mzenga ameonyesha umahiri wake katika kujenga na kuendeleza maudhui. Jambo hili limetufaulisha katika kuchnganua maudhui ya ushujaa, dini, miujiza, malezi na nafasi ya wanawake, sharia za torati, ndoa, maadili, usaliti na dhuluma, pamoja na kifo na ufufukaji katika kazi yake. Licha ya kuwa maudhui haya ni ya jadi, bado yana uamilifu kwa sababu yameakisi hali yakinifu katika jamii ya sasa.

Vilevile tumeweza kugundua kuwa kulingana na utenzi huu, binadamu hana uwezo wa kujiamulia hatima yake ya uzazi, yaani, uwezo hana wa kuamua kuzaa mwana wa kike au wa kiume, yote ni kwa uamuzi wa Mola kulingana na mtazamo wetu kutokana na *Utenzi wa Nabii Isa*, hii ndiyo sababu ya Mola kuwapa Bwana Imrani na mkewe mwana wa kike hata ingawa walimwomba Mola mwana wa kiume (beti 28-29) au hata uamuzi wa kuzaa mwana bila baba kama ilivyo hali ya uzazi wa Nabii Isa kwa Mariyamu malaika anapomhakikishia Mariyamu kuwa uzazi wake hautahusu mume (ubeti 147).

Pia tumegundua kuwa, maudhui yamefaulishwa na mihimili ya kifani ambayo imekuwa nguzo ya kuyasitiri, kutoka mwanzo wa kisa hiki hadi mwisho, na daima vipengele hivi

viwili hutegemeana pakubwa. Katika utafiti wetu huu, hatujaweza kutenga maudhui na fani licha ya kuwa maudhui hayo ndiyo yaliyokuwa tatizo letu la utafiti.

## 5.3 KUHUSU NADHARIA TETE.

Utafiti wetu ulihusu nadhari tete nne:

Mwanzo, tulichukulia kuwa mtunzi wa *Utenzi wa Nabii Isa* anafahamu hali yakinifu ya wanajamii anaowatungia kazi hii kwani ameangazia shughuli zao za kila siku. Tumeonyesha jinsi uzoevu wake umemwezesha kupata malighafi kutokana na jamii ili kuibua maudhui ya ushujaa, ndoa, dini, usaliti na dhuluma, miujiza, malezi na nafasi ya wanawake, sharia za torati, maadili na kifo na ufufukaji.

Pia tumethibitisha kuwa kulingana na *Utenzi wa Nabii Isa*, mwanamke hana nafasi ya kuamua hatima yake kuhusu swala la uzazi. Aidha, hawezi kuamua kuzaa mwana wa kike au wa kiume, kupata mtoto au kutopata. Bwana Imrani na mkewe waliomba mola awape mwana wa kiume lakini Mola akawajalia na mwana wa kike (Mariyamu), kwingine, Mariyamu anapata mimba na kuzaa mwana (Nabii Isa) bila kukutana na mume kimwili. Hii inaonyesha kuwa hana uamuzi wa; ni lini apate mtoto kwa sababu ya nafasi ya Mola kuwa ndiye muweza na anaamua kumpa mwana kabla ya matarajio yake.

Tatu, tumeonyesha kuwa majagina ni mfano mwema wa kuonyesha uhalisia wa kiajabu katika jamii kwani wana sifa sufufu za kiajabu zinazowatambulisha kama mashujaa hasa tukijikita katika usawiri wa wahusika katika *Utenzi wa Nabii Isa* kama Nabii Isa na mtume Musa.

Mwisho ni kuwa, maudhui teule katika utenzi huu yamejengeka na kupelekwa mbele na kuunda ploti za kazi nzima ambayo ina mnato kwa wasomaji kwa kutumia mihimili ya kifani ambayo imeyasitiri vilivyo. Kwa hivyo, nadharia tete zetu zimefaulu kwani zimekuwa na mashiko.

## 5.4 MAPENDEKEZO YA UTAFITI ZAIDI.

Utafiti huu wetu umeshughulikia uchanganuzi wa maudhui teule katika *Utenzi wa Nabii Isa.* Hata hivyo, hatuwezi kikiri kuwa tumeshughulikia swala hili katika ukamilifu wake wala hakuna yeyote anayeweza kudai kwamba amefanya utafiti ambao umekamilika kuhusu kazi ya kifasihi.

Fasihi ina mambo mengi ya kuchunguzwa na kwa misingi hii, kuna mambo mengine mengi ya kufanyiwa uchunguzi kuhusu maudhui katika *Utenzi* wa *Nabii Isa.* Tunapendekeza utafiti ufanywe zaidi kuhusu *Utenzi wa Nabii Isa* kimaudhui.

Utafiti wetu huu wa ushairi wa Kiswahili umetoa mchango katika kulijaza pengo lililokuwepo la kukosa uhakiki wa kimaudhui wa *Utenzi wa Nabii Isa* kwa misingi ya nadharia ya Uyakinifu wa Kijamii. Mchango huu ni muhimu kwa kuwa swala hili na nadharia hii ni mambo yanayofaa tafiti za baadaye katika uwanja wa fasihi ya Kiswahili na iwapo kuna swala ambalo hatujashugulikia hapa tunaomba watafiti na wahakiki wengine waangazie zaidi.

## 5.5 HITIMISHO.

Hii ni sura ya mwisho na ndiyo imehitimisha mradi wetu wa utafiti. Katika sura hii, tumetalii baadhi ya vipengele muhimu vya kuhakiki matokeo ya utafiti wetu kama vile kutoa muhtasari wa utafiti wetu, kutathmini matokeo ya malengo ya utafiti, maelezo kuhusu matokeo ya nadharia tete na mwishowe tumependekeza utafiti zaidi kuhusu mada yetu "*Uhakiki wa Maudhui teule katika Utenzi wa Nabii Isa."*

## MAREJELEO


Achebe (1975): *Morning Yet on Creation Day.* London: Heinmann.

Achieng (2012): *Sifa za Mashujaa na Umuhimu wao kwa Jamii zao: Ulinganifu wa Fumo Liyongo na Lwanda Magere*. Tasnifu ya Uzamili ya Chuo kikuu cha Nairobi ambayo bado haijachapishwa.

Biblia (2010): *Agano Jipya*, India: Gideons International.

Casey (2004): *Unlikely Heroes and their roles in Fantasy Literature*, mswada ambao bado haujachapishwa.

Ellen (2001): *The desire of Ages.* Herald Publishing House.

Gatakaa (2012): *Uhakiki wa Maudhui Teule katika Utenzi wa Mikidadi na Mayasa*. Tasnifu ya Uzamili. Chuo kikuu cha Nairobi ambayo bado haijachpishwa.

Gorky (1973): *The Lower Division*, The Vikings Press.

Harries (1962): *Swahili Poetry:* Oxford: The claredon Press.

Http / google (2013): *The Classic Literary Hero*, Mswada ambao haujachapishwa.

Http / google (2005): Al Islam.Org/Kiswahili vitabu:*Usahihi wa Historia ya Uislamu na Waislamu.* mswada ambao haujachapishwa.

Knappert (1967): *Traditional Swahili Poetry: An Investigation into the Concepts of East African Islam as reflected in the Utenzi Literature*, E.J. Brill, Leiden.

Lucaks (1963*): The meaning of contemporary realism*, London: Merlin Press.

Mbatiah (2010): *Mwendawazimu na Hadithi Nyingine: Mambo muhimu katika uhakiki wa Hadithi fupi.* Jomo Kenyatta Foundation.

Mdee nw (2011): *Kamusi ya karne ya 21*, Longhorn Publishers.

Mungai, P (2005): "*Ulinganishi wa kifani wa tenzi za Swifa ya Nguvumali na Mikidadi na Mayasa".* Tasnifu ya Uzamili ya Chuo Kikuu Cha Nairobi ambayo bado haijachapishwa.

Mzenga (1977): *Utenzi wa Nabii Isa*, Nairobi: Foundation Books Limited.

Njogu na Chimera (1999): *Ufundishaji wa Fasihi: Nadharia na mbinu*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Orwell, G (1967): *Shamba La Wanyama*. Nairobi: Kenya Litho Limited.

Swaleh, A (1992): "*Maudhui katika Utenzi wa Mwanakupona*". Tasnifu ya uzamili ya Chuo Kikuu cha Nairobi ambayo bado haijachapishwa.

Tuki (2004): *Kamusi ya Kiswahili sanifu*. Oxford University Press.

Wa Mberia (1989): "Fumo Liyongo", Mulika nambari ya 21 uk 25-43.

Wamitila K, W (2002): *Uhakiki wa Fasihi-Misingi na Vipengele vyake,* Nairobi: Phoenix publishers.

Wa Mberia (2003): *Kamusi ya Fasihi-Istilahi na Nadharia*, Nairobi: Focus Publishers.

Wa Mberia (2008): *Kanzi ya Fasihi-Misingi ya Uchanganuzi wa Fasihi*, Nairobi: Vide Muwa Publishers.

Wamitila (2002): *Uhakiki wa Fasihi*: Misingi na vipengele vyake. Nairobi: Phoenix Publishers Limited.

Wamitila (2008): *Kanzi ya Fasihi: Misingi ya Uchanganuzi wa Fasihi*. Nairobi: Vide – Muwa Publishers Limited.

Wa Mutiso (1985): *Hurafa na uyakinifu katika utenzi wa Hamziyya.* Tasnifu ya uzamili ya Chuo kikuu cha Nairobi ambayo bado haijachapishwa.

Werner (1932): *Hadithi ya Mikidad na Mayasa*. Amedstead Hemsphire: The Azania Press